**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

# HOTUBA YA MAKADIRIO NA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**ILIYOWASILISHWA NA**

**MHESHIMIWA HEMED SULEIMAN ABDULLA**
**MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR**
**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR**

**ZANZIBAR** **MEI, 2024**



**MHESHIMIWA HEMED SULEIMAN ABDULLA**
**MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR**



**MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA**
**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS,**
**(SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI)**



**DKT. ISLAM SEIF SALUM**
**KATIBU MKUU OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS,**
**(SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI)**

## Dira

*“ Kuwa na Serikali yenye kutoa huduma bora kwa jamii na yenye uhimili mzuri wa uchumi, umoja na maendeleo endelevu”*

## Dhamira

*“Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali katika sekta zote za SMZ na masuala ya Muungano kwa kufuata misingi ya Katiba na Sheria pamoja na kufuata misingi ya haki za binaadamu na ushirikishwaji”.*

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na hatimae likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima na afya. Na kwa uwezo wake na kadari yake ameendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani na utulivu mkubwa. Tunamuomba atuzidishie mshikamano na upendo miongoni mwetu ili tuendelee kuidumisha amani hiyo.

3. **Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni nchi yetu ilipata misiba miwili mikubwa ya Kitaifa ambapo tarehe 10 Februari, 2024 Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mstaafu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowasa alifariki dunia na tarehe 29 Februari, 2024 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mstaafu, Mheshimiwa Mzee Ali Hassan Mwinyi alifariki dunia. Naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wananchi wa Zanzibar kuendelea kutoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na wananchi wote wa Tanzania na kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi na wananchi wote wa Zanzibar kutokana na vifo hivyo vya waliokuwa viongozi wetu wa Kitaifa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hao mahala pema peponi….*Amin.*

4. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara wenye kuleta maendeleo kwa Watanzania wote. Aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa namna anavyoiongoza nchi yetu na kutuwekea mazingira mazuri ya utendaji kazi ili kufikia malengo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awazidishie nguvu, hekima na busara viongozi wetu hawa ili waendelee kuiongoza vyema nchi yetu na kufikia maendeleo tuliyoyadhamiria.

5. **Mheshimiwa Spika,** nachukua nafasi hii kuwapongeza Viongozi wetu hawa kwa kuadhimisha Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar na Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sote tumeshuhudia sherehe zilizofana ambazo ziliambatana na uwekaji wa mawe ya msingi na ufunguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

6. **Mheshimiwa Spika,** pongezi na shukrani nyingi nazileta kwako wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa namna unavyoendelea kuliongoza na kulisimamia Baraza hili Tukufu kwa kushirikiana na wasaidizi wako Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza. Mwenyezi Mungu azidi kukupeni nguvu na uwezo wa kuliendesha Baraza hili ili lifikie azma yake.

7. **Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa napenda kutoa shukurani kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mheshimiwa Machano Othman Said na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Maryam Thani Juma pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo, kwa kuendelea kutushauri na kutupa miongozo mbalimbali juu ya shughuli tunazozitekeleza au tunazopanga kutekeleza. Ushauri na miongozo yao imekuwa na mchango mkubwa katika mipango

na mafanikio yetu ya kiutekelezaji. Vilevile, tunawashukuru kwa kuipitia na kuijadili kwa kina hotuba hii na hatimae kuipitisha baada ya kupata ufafanuzi wa hoja mbalimbali walizozitoa.

8. **Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu naomba niwapongeze Waheshimiwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti pamoja na Wajumbe wa Kamati zote za Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanazozifanya za kusimamia kazi za Wizara na sekta zote za Serikali ili kuhakikisha utekelezaji mzuri na wenye tija kwa Serikali na jamii kwa jumla. Ni ukweli usiofichika kuwa sisi Serikali tuna matumaini makubwa na Kamati hizi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza kwa jumla kwa namna mnavyoendelea kuwatumikia wananchi kwa lengo la kuleta maendeleo kwa manufaa ya nchi yetu.

9. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi huo wa salamu za pole, shukurani na pongezi kwa ridhaa yako naomba nieleze kwa muhtasari hali ya mafanikio pamoja na mipango ya Serikali katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa ujumla katika nchi yetu.

**MWENENDO WA UCHUMI WA ZANZIBAR**

10. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023 uchumi wa Zanzibar umeendelea kuwa imara na kufikia ukuaji wa wastani wa **asilimia 7.4**, ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa **asilimia 6.8** mwaka 2022. Miongoni mwa mambo yaliyochangia kuimarika kwa ukuaji wa uchumi ni:

   i. Kuimarika kwa Sekta ya Huduma ambayo imekua na kufikia wastani wa **asilimia 9.9** mwaka 2023 kutoka wastani wa **asilimia 7.7** mwaka 2022. Ongezeko hili kwa kiasi kikubwa limetokana na kuongezeka kwa watalii waliotembelea Zanzibar ambao wamefikia watalii 638,498

mwaka 2023 kutoka watalii 548,503 mwaka 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 16.4;**

ii. Kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji kufikia miradi 114 yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 4.64** mwaka 2023 kutoka miradi 93 yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 4.55** mwaka 2022;

iii. Kuongezeka kwa thamani ya zao la Mwani kufikia **Shilingi Bilioni 19.23** mwaka 2023 kutoka **Shilingi Bilioni 16.01** mwaka 2022;

iv. Kuendelea kuwepo kwa hali ya amani na utulivu nchini jambo ambalo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

**Pato la Taifa na Pato la Mwananchi**

11. **Mheshimiwa Spika,** Pato halisi la Taifa (GDP at constant price) limeongezeka na kufikia thamani ya **Shilingi Bilioni 3.75** mwaka 2023 kutoka thamani ya **Shilingi Bilioni 3.49** mwaka 2022. Vile vile, Pato la Taifa kwa bei ya soko (GDP at current price) limeongezeka na kufikia thamani ya **Shilingi Bilioni 6.04** mwaka 2023 kutoka thamani ya **Shilingi Bilioni 5.40** mwaka 2022. Kuongezeka kwa Pato la Taifa kumepelekea kuongezeka Pato la mwananchi kufika **Shilingi Milioni 3.1** (USD 1,241) kutoka **Shilingi Milioni 2.8** (USD 1,235) kwa mwaka 2022.

**Mfumko wa Bei**

12. **Mheshimiwa Spika,** kasi ya mfumko wa bei kwa mwaka 2023 imeongezeka na kufikia wastani wa **asilimia 6.9** kutoka wastani wa **asilimia 5.1** mwaka 2022. Kuongezeka kwa kasi ya mfumko wa bei kumetokana na ongezeko la bei za bidhaa za chakula katika soko la ndani. Kwa mwaka 2023, bidhaa za chakula zimeongezeka na kufikia wastani wa **asilimia 11.1** kutoka wastani wa **asilimia 6.0** mwaka 2022. Uagizaji

wa bidhaa kutoka nje ya nchi ndio sababu kuu ya kupanda kwa bei za bidhaa za chakula kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa hizo katika soko la dunia. Hata hivyo, kwa bidhaa zisizo za chakula kasi ya mfumko wa bei ilipungua kufikia wastani wa **asilimia 4.0** mwaka 2023 kutoka wastani wa **asilimia 4.5** mwaka 2022 kutokana na Serikali kufidia gharama za ziada kwa bidhaa za nishati ya mafuta..

### Hatua za Kudhibiti Mfumko wa Bei

13. **Mheshimiwa Spika,** katika kudhibiti hali ya mfumko wa bei, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi; kuimarisha programu za kilimo ili kuongeza uzalishaji wa ndani; kuendelea kudhibiti mwenendo wa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT); kuimarisha ufanisi wa Bandari ya Malindi kwa ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kupunguza muda wa kutoa mizigo bandarini na kufunguliwa kwa bandari nyengine ya utoaji mizigo Fumba.

14. **Mheshimiwa Spika,** lengo la hatua zote hizi ni kupunguza ukali wa bei za bidhaa na huduma kwa wananchi pamoja na kurahisisha upatikanaji wa bidhaa na huduma hizo. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia na kufuatilia mwenendo mzima wa biashara ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata nafuu katika mzunguko mzima wa biashara nchini.

### Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2024

15. **Mheshimiwa Spika,** mwelekeo wa hali ya uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2024 unakwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2050, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021-2026) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020.

16. **Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.6 mwaka 2024 kutokana na sababu zifuatazo:

i. Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii watakaotembelea Zanzibar kutokana na kuimarisha vivutio vya utalii na miundombinu wezeshi;

ii. Kuendelea kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya barabara za mjini na vijijini, ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo miundombinu ya afya, elimu, maji safi na salama na ujenzi wa viwanja vya michezo kwa kila Wilaya;

iii. Kuendelea na hatua za kudhibiti kasi ya mfumko wa bei ili kubakia katika tarakimu moja;

iv. Kuongezeka kwa usimamizi wa ukusanyaji wa mapato pamoja na udhibiti wa matumizi ya Serikali;

v. Kuongezeka kwa hatua za kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza miradi binafsi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje;

vi. Kuongeza usimamizi wa miradi ya Kimkakati; na

vii. Kuimarisha shughuli za uchumi wa buluu kupitia usajili wa kampuni za kimataifa za uvuvi na viwanda vya usindikaji wa samaki na mazao ya baharini.

## MAENDELEO YA SEKTA MBALIMBALI

### Sekta ya Usafirishaji na Mawasiliano

17. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya usafirishaji na mawasiliano ni miongoni mwa sekta muhimu katika kuwezesha ukuaji wa uchumi wa nchi pamoja na upatikanaji wa huduma za kijamii. Serikali imedhamiria kuendelea kuimarisha sekta hii kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na uimarishaji

wa miundombinu ikiwemo bandari zetu za Mangapwani, Mkokotoni, Shumba Mjini, Mkoani, Wete na Fumba.

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ujenzi wa Bandari ya Mangapwani, Serikali inaendelea kuweka miundombinu mbalimbali ikiwemo barabara zenye urefu wa kilomita 12 ambapo ujenzi wa barabara hizo umefikia **asiliamia 35.** Aidha, Serikali imo katika hatua za mwisho za kuingia makubaliano na Kampuni ya China Harbour Engineering Company (CHEC) katika ujenzi wa Bandari hiyo baada ya kufanyiwa mapitio ya upembuzi yakinifu na Kampuni ya Ushauri elekezi ya Dar Handasar ili kuhakikisha Mradi wa Ujenzi wa Bandari hiyo unaanza ndani ya mwaka wa fedha 2024/2025.

19. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uimarishaji wa Bandari ya Mkokotoni, Serikali tayari imejenga Jengo la Abiria lenye uwezo wa kuchukua watu 250, ghala la mizigo pamoja na njia ya kupita abiria wakati wa kuelekea kwenye chombo. Aidha, ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini ambayo baada ya kukamilika itakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria na mizigo pamoja na meli zenye uzito wa tani 2,000 unaendelea vizuri. Kazi za ujenzi zimefikia **asilimia 17** na unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2024/2025.

20. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha Bandari ya Mkoani na kukamilisha matengenezo sehemu ya kuhifadhi Makontena (Container Yard) yenye ukubwa wa mita za mraba 4,200 na uzio wenye mfumo wa usalama wa umeme wenye uwezo wa kuhifadhi makontena 580. Kuweka njia ya kupitia abiria yenye urefu wa mita 300 na upana wa mita 2.5. Aidha, imefanya utanuzi wa njia kwa ajili ya kuwezesha vitendea kazi kama Reach Stacker, Crane na Terminal Tractor kupita, kujenga ukuta wa kuzuia mmong'onyoko wa udongo (Retaining Wall) wenye mita 120; pamoja na kukarabati gati (Jetty).

21. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Serikali inaendelea na mpango wake wa kuimarisha Bandari ya Wete ambapo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali (Feasibility Study and Preliminary Engineering Design) imemalizika. Kazi hiyo imefanywa na Mshauri elekezi Inros Lackener kutoka Ujerumani ambae pia ametayarisha mchoro unaoonesha mwelekeo mpya wa Bandari hiyo.

22. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Fumba ni uwekezaji uliofanywa kwa kuzingatia matakwa ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2,050 inayotoa nafasi kwa sekta binafsi kuendesha shughuli za bandari. Kampuni ya Fumba Inland Container Depot Limited ilipatiwa eneo la uwekezaji kwa mujibu wa taratibu kupitia Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) lenye ukubwa wa hekta 4.96. Kampuni hiyo imefanya ujenzi wa bandari kavu yenye uwezo wa kuchukua makontena 3,000 TEUS pamoja na sehemu ya kuegesha meli. Aidha, Kampuni hiyo iliendelea na uwekaji wa mifumo ya kielektroniki itakayowezesha kutoa huduma kwa ufanisi mkubwa. Tayari huduma ya kushusha makontena imeanza kutolewa katika bandari hiyo.

23. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Usafiri wa Anga, Serikali inaendelea na azma yake ya kuimarisha huduma za sekta hiyo kwa kuboresha miundombinu na mifumo katika viwanja vyetu vya ndege. Hivi sasa taratibu za ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba zimekamilika na hivi karibuni shughuli za ujenzi wa uwanja huo zitaanza rasmi. Aidha, ujenzi wa jengo jipya la pili la abiria (Terminal II) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume tayari umeshaanza na unategemewa kukamilika ndani miezi 30. Tunaamini kukamilika kwa miradi hiyo kutazidi kuupatia heshima Uwanja wetu Kimataifa na Serikali kwa jumla baada ya hivi karibuni kupata tuzo kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kuwa ni Uwanja bora barani Afrika unaotoa huduma bora kwa abiria

chini ya milioni mbili kwa mwaka. Wito wangu kwa viongozi, watendaji na watoa huduma wote wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kuendelea kusimamia utoaji wa huduma ulio bora ili tuzidi kupata heshima kwa viwanja vyetu na nchi kwa jumla.

24. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuweka umuhimu katika suala la mawasiliano kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma za kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Hali halisi ya upatikanaji wa huduma ya mawasiliano ya simu hivi sasa ni asilimia 100 katika maeneo yote yenye makaazi ya watu. Hii ikiwa ni zaidi ya lengo la asilimia 80 iliyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 katika Ibara ya 61(f).

25. **Mheshimiwa Spika,** Serikali hivi sasa imeweka nguvu kubwa katika uimarishaji wa miundombinu ya barabara mijini na vijijini, Unguja na Pemba. Miongoni mwa barabara hizo ni Barabara ya Wete – Chake yenye urefu wa kilomita 22.1, Barabara ya Tunguu - Makunduchi (km 48.5), Barabara ya Fumba – Kisauni (km 12) na Barabara ya Mkoani – Chakechake (km 43.5). Serikali tayari imekamilisha taratibu zote za ujenzi wa barabara hizi na tayari malipo ya awali yameshafanyika kwa wakandarasi wanaohusika. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza hivi karibuni ukiacha barabara ya Wete – Chake ambayo kazi ya ujenzi imeshaanza na inaendelea.

26. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na ujenzi huo, Serikali imepanga kuendelea na ujenzi wa barabara za Mjini zenye urefu wa kilomita 100.9 ambazo zitajumuisha misingi ya maji, njia za waenda kwa miguu na taa za barabarani kwa lengo la kubadilisha haiba ya mji wetu wa Zanzibar. Aidha, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa barabara mpya zenye urefu wa kilomita 277 Unguja na Pemba ikiwa ni sehemu ya barabara ambazo zimo katika Ilani ya Uchaguzi ya ya CCM ya mwaka 2020. Tunawaomba wananchi wote wa maeneo

yatakayohusika na ujenzi wa barabara hizo kutoa ushirikiano mkubwa kwa wakandarasi wetu ili shughuli za ujenzi ziweze kufanyika kwa ufanisi mkubwa na kukamilika kwa wakati. Aidha, napenda niwasisitize waendelee kuwa na ustahamilivu wakati wote ambao ujenzi unaendelea.

**Sekta ya Uchumi wa Buluu**

27. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuweka mkazo katika uimarishaji wa Sekta ya Uchumi wa Buluu ili kuhakikisha ongezeko kubwa la tija kwa wananchi na Serikali kutokana na sekta hiyo. Tayari kwa mwaka 2023 kuna ongezeko kubwa la kiwango cha uzalishaji wa samaki kilichofikia tani **80,085** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 569.07** kutoka **tani 61,794** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 391.37** mwaka 2022. Hili ikiwa ni ongezeko la **asilimia 29.5.** Vilevile, uzalishaji wa zao la mwani umeongezeka kutoka tani **12,594** mwaka 2022 hadi kufikia **tani 16,653** mwaka 2023 sawa na ongezeko la **asilimia 32.2.**

28. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuchukua jitihada kubwa ya kuweka mifumo ya kitaasisi ili kuifanya sekta hii kuendelea kuwa tegemeo katika kukuza uchumi wa wananchi na nchi kwa jumla. Miongoni mwa jitihada hizo ni kuwa na sera na sheria ambazo zitatumika katika utekelezaji na uendelezaji wa shughuli za uchumi wa buluu ikiwemo Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini ambayo tayari imeshasainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Aidha, Serikali imezindua rasmi Sera zake za Uchumi wa Buluu pamoja na Mkakati Wake wa Utekelezaji, Sera ya Uvuvi pamoja na Mkakati Wake wa Utekelezaji, Mpango Mkuu wa Uvuvi, pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wa Ukondoishaji wa Masuala ya Kijinsia katika Uchumi wa Buluu (Gender Action Plan on Blue Economy). Aidha, Serikali imeendelea

kufanya tafiti zinazohusiana na sekta hii ili kuleta mageuzi na maendeleo zaidi ya kisekta.

**Huduma ya Maji Safi na Salama**

29. **Mheshimiwa Spika,** lengo la Serikali katika upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama mijini na vijijini ni kufikia zaidi ya **asilimia 85** ifikapo mwaka 2025. Kwa sasa hali ya uzalishaji maji imefikia wastani wa **asilimia 75** ukilinganisha na **asilimia 67** iliyofikiwa mwaka jana. Ingawa tunaendelea vyema katika kufikia asilimia tuliojiwekea, bado kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazohusiana na upatikanaji wa huduma hiyo. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuongezeka kwa mahitaji ya maji ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024, mahitaji ya maji yamefikia lita 275,980,481 kwa siku kutoka lita 240,465,120 wakati uzalishaji kwa sasa ni lita 206,067,422.

30. **Mheshimiwa Spika,** Miradi mbalimbali inaendelea kutekelezwa ili kukabiliana na changamoto hizo ikiwemo Miradi ya Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji na Programu ya Ahueni ya Uviko-19. Kupitia miradi hiyo jumla ya visima vipya 102 vimechimbwa vyenye uwezo wa kuzalisha lita 201,552,000 kwa siku, ujenzi wa matangi 25 makubwa ya kuhifadhia maji lita 144,000,000 pamoja na kuweka mtandao wa maji kwa masafa ya kilomita 785.9.

31. **Mheshimiwa Spika,** ni matarajio yetu kuwa baada ya kukamilika na kufanyakazi kwa miundombinu hii ya uzalishaji na usambazaji maji safi na salama, uzalishaji maji unatarajiwa kufikia lita 430,737,222 kwa siku. Hivyo tatizo la maji nchini litapungua kwa asilimia kubwa. Naomba wananchi waendelee kuiunga mkono Serikali katika utekelezaji wa miradi hii ili tuweze kufanikiwa na kifikia lengo tulilojiwekea.

**Huduma za Nishati**

32. **Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na ongezeko la mahitaji ya umeme kwa ajili shughuli za kijamii na kiuchumi. Mahitaji ya juu ya umeme (Peak demand) kwa upande wa Unguja yamefikia Megawati **119.3** ikiwa ni ongezeko la Megawati **14.4** lililofikiwa mwaka jana. Matumizi katika waya wa Megawati **100** yamefikia Megawati **90.3,** ikiwa ni ongezeko la Megawati 7.3 na waya wa megawati **45** yalifikia megawati **29** sawa na ongezeko la Megawati **7.1** ikiwa ni **asilimia 82** ya uwezo wa waya mbili zilizopo. Aidha, kwa upande wa Pemba mahitaji ya juu ya umeme ni Megawati **11.24** sawa na **asilimia 56** ya uwezo wa waya unaotumika hadi sasa wa Megawati **20.**

33. **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na ongezeko hilo la mahitaji ya nishati ya umeme, Serikali imeshaanza hatua za uwekezaji wa uzalishaji wa nishati mbadala ya umeme wa jua. Serikali tayari imesaini makubalino ya mauziano ya umeme na kampuni mbili zitakazozalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua. Kampuni hizo ni Generation Capital Limited ambayo itaanza kwa kuzalisha kiwango cha Megawati **30** katika kisiwa cha Unguja na Kampuni ya ESR ya Ujerumani ambayo itaanza uzalishaji wa Megawati **15** katika Kisiwa cha Pemba. Hatua hii inaenda sambamba na uimarishaji wa upatikanaji wa kiwango kizuri cha umeme na kuondoa changamoto ya umeme mdogo hapa nchini.

34. **Mheshimiwa Spika,** niwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa jumla, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuibua na kutekeleza miradi itakayopunguza au kuondosha kabisa changamoto zinazopelekea upatikanaji hafifu wa huduma hii muhimu ya nishati ya umeme hapa nchini.

**Huduma za Afya**

35. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuiweka sekta ya afya kuwa ni miongoni mwa sekta muhimu katika ustawi wa nchi yetu. Serikali inachukua kila jitihada na kuweka mikakati ya kuimarisha huduma za mama na mtoto ili kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga. Imeimarisha huduma za kliniki ikiwemo huduma za upimaji na chanjo kabla na baada ya kujifungua. Tunaamini kuwa kuimarika kwa huduma za upimaji na chanjo wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua kutaimarisha afya ya mama na mtoto kutokana na ufuatiliaji wa karibu wa maendeleo ya mtoto na ushauri unaotolewa kwa mama wajawazito. Napenda kutoa wito kwa kina baba wenzangu kushirikiana na wenza wetu wakati wa mahudhurio ya kliniki ya mama na mtoto ili kujua maendeleo ya afya zao pamoja na kupata elimu ya lishe bora na namna bora ya kuwahudumia.

36. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha miundombinu ya afya, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya uhakiki wa vituo vyote vya afya ili kubaini uwezo na mgawanyo wa vituo hivyo kwa maeneo sambamba na huduma zinazotolewa. Matokeo ya uhakiki huo yalionesha kuwa kati ya vituo **173,** vituo **142** (Dispensari **90** na Vituo vya Afya **52**) vinahitajika kutoa huduma za afya ya msingi kwa mujibu wa miongozo ya utoaji wa huduma za afya. Aidha, jumla ya vituo vya afya **39** vinatakiwa kufanyiwa matengenezo madogo, vituo **18** vinatakiwa kufanyiwa matengenezo makubwa na vituo **85** vinatakiwa kujengwa upya.

37. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imezingatia uhakiki huo na kuanza kuufanyia kazi ambapo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga jumla ya **Shillingi Bilioni 35** za kuendeleza ujenzi na kuimarisha vituo vipya.

38. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha huduma ya upatikanaji wa dawa muhimu katika hospitali na vituo vya afya vya Serikali na hospitali ambazo zinaendeshwa na makampuni binafsi. Upatikanaji wa dawa hizo umefikia **asilimia 90** kwa hospitali na kwa upande wa vituo vya afya umefikia **asilimia 73.** Lengo la Serikali ni kuhakikisha upatikanaji wa dawa unafikia **asilimia 100** kwa maeneo yote.

**Sekta ya Elimu**

39. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya elimu na kuweka mazingira mazuri kwa wanafunzi na walimu kuweza kupata elimu. Katika kipindi hiki Serikali imejenga skuli 26 za ghorofa Unguja na Pemba ili kuwawezesha wanafunzi kupata elimu katika mazingira mazuri. Miongoni mwa skuli zilizokamilika na kufunguliwa rasmi ni Skuli ya Fuoni na Skuli ya Muembeladu Unguja sambamba na Skuli tano (5) zilizofunguliwa wakati wa Maadhimisho ya Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Skuli hizo ni Skuli ya Donge na Skuli ya Mtopepo, Skuli ya Utaani, Skuli ya Maziwang'ombe na Skuli ya Kiwani. Ujenzi wa skuli **19** unaendelea na unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka huu wa 2024.

40. **Mheshimiwa Spika,** kwa azma ileile ya kuimarisha ubora wa elimu na kuweka mazingira bora ya kujifunza na kufundisha, Serikali imeanza utekelezaji wa miradi miwili mipya yenye thamani ya Dola za Kimarekani **Milioni 60.17.** Miradi hii imelenga katika kuimarisha ubora wa elimu ya lazima kwa kuwapatia walimu mafunzo, kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, matumizi ya TEHAMA katika elimu pamoja na kuimarisha miundombinu ya skuli kwa kujenga skuli 7 mpya Unguja na Pemba.

41. **Mheshimiwa Spika,** uwekezaji huu katika sekta ya elimu umetuonesha matunda yake kwani hali ya ufaulu kwa vijana

wetu wanaofanya mitihani ya Taifa imekuwa ya kiwango cha juu. Ufaulu wa wanafunzi kwa mtihani wa Kidato cha Sita uliofanyika Mei, 2023 ulikuwa ni kwa **asilimia 99.92** ambapo jumla ya watahiniwa **2,585** walifaulu kati ya watahiniwa **2,587.** Aidha, wanafunzi **20,976** wamefaulu mitihani yao ya Kidato cha Nne mwaka 2023 ikiwa ni sawa na asilimia 85.9 ya watahiniwa wote **24,420** waliofanya mtihani huo.

**42.** **Mheshimiwa Spika,** mipango ya Serikali katika sekta hii ya elimu ni kuendelea kuimarisha mfumo wa tathmini ya maendeleo ya elimu katika ngazi zote za elimu na kupandisha ufaulu wa wanafunzi; Kuimarisha miundombinu ya elimu kwa kujenga Skuli za ghorofa, Ofisi za Elimu za Wilaya, nyumba za walimu, dakhalia pamoja na kuzifanyia ukarabati mkubwa na mdogo skuli 100 Unguja na Pemba.

**Uendelezaji wa Matumizi ya Ardhi**

**43.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali yetu imeazimia kupunguza na kuondoa matumizi holela ya ardhi kwa kusimamia sera na kanuni zinazoongoza mipango na matumizi ya ardhi hapa nchini. Serikali imefanya kazi kubwa ya upimaji wa viwanja 1,375 (843 Unguja na 568 Pemba). Maeneo yaliyopimwa ni maeneo ya makaazi, taasisi, mashamba, eka na maeneo ya vitega uchumi. Aidha, Serikali imeandaa Hati za Matumizi ya Ardhi 880 (Unguja 614 na Pemba 266) sambamba na kuimarisha upatikanaji wa Mikataba ya Ukodishwaji Ardhi 278 (Unguja 257 na Pemba 21) kwa lengo la kuendeleza sekta ya uwekezaji nchini. Serikali hivi sasa inaandaa Mpango Maalum wa Matumizi ya Ardhi ambao utasaidia udhibiti wa matumizi ya ardhi kama yalivyopangwa kwa kuainisha matumizi maalum kwa ajili ya Makaazi, uwekezaji, Kilimo, Maeneo ya Hifadhi na maeneo huduma nyengine za kijamii.

**44.** **Mheshimiwa Spika,** tumekuwa tukishuhudia migogoro mingi ya ardhi katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Serikali

imeendelea kuchukua kila hatua na jitihada kuhakikisha migogoro hiyo inamalizika kwa usalama na kwa maridhiano. Kupitia Kamati Maalum ya Usuluhishi wa Migogoro ya Ardhi, jumla ya migogoro 35 tayari imepatiwa ufumbuzi kati ya migogoro 76 iliyowasilishwa ikiwa ni sawa na **asilimia 46.1**.

## SEKTA ZA UZALISHAJI NA UWEKEZAJI

### Sekta ya Kilimo

45. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya kilimo ni moja ya sekta zinazowagusa moja kwa moja wananchi hasa katika suala la uzalishaji na upatikanaji wa chakula. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kuipa kipaumbele sekta hii na kuhakikisha wananchi wanapata chakula cha kutosha na kilicho bora kutokana na shughuli za kilimo na ufugaji. Serikali imeendelea kufanya tafiti mbalimbali hasa za mazao ili kuweza kutatua changamoto zinazowakabili wakulima na wafugaji katika shughuli zao. Hivi karibuni Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mpunga (International Rice Research Institute – IRRI) imefanya tafiti za kudhibiti maradhi ya ukungu kwa mpunga (rice blast) na michirizi ya manjano katika mpunga (rice yellow mottle diseases). Tafiti hizo zinaendelea katika maeneo ya Kibonde Mzungu, Mwera na Bumbwisudi kwa Unguja na Tungamaa kwa Pemba ili kujiridhisha na uimara wa mbegu za mpunga zilizochaguliwa katika kustahamili mashambulizi ya maradhi hayo kabla ya kupelekwa rasmi kwa wakulima kwa ajili ya uzalishaji.

46. **Mheshimiwa Spika,** Aina 4 za migomba iliyozalishwa kwa njia ya maabara (tissue culture) zilizoripotiwa kupatikana mwaka jana zinaendelea kuzalishwa na kusambazwa kwa wakulima. Hadi sasa jumla ya miche 196 imetolewa kwa wakulima 26 katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba ili kuangalia ukuaji na uzalishaji katika mazingira tofauti.

47. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekamilisha kazi ya kupima afya ya udongo wa mashamba ya wakulima ili kujua hali ya rutuba na uwezo wa kuzalisha mazao mbali mbali. Sampuli za udongo 500 zilichukuliwa na kupimwa na tayari majibu ya uchunguzi huo yameshapatikana na kukabidhiwa kwa wakulima pamoja na mapendekezo ya kutatua changamoto zilizogunduliwa. Kazi hiyo itakuwa ni endelevu na itakwenda sambamba na utoaji wa elimu juu ya uhifadhi wa rutuba kwa wakulima. Jumla ya wakulima 2,000 wa Unguja na Pemba wanatarajiwa kupatiwa elimu na kupimiwa afya ya udongo wa mashamba yao katika mwaka huu wa 2024/2025.

48. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uzalishaji na ubora wa karafuu zinazozalishwa Zanzibar, Serikali kwa kushirikiana na Kituo cha Maendeleo ya Utafiti wa Kilimo cha Ufaransa (CIRAD) imefanya utafiti wa kutambua vinasaba vya karafuu ya Zanzibar (Zanzibar clove genetic diversity) ambao matokeo yake yanatarajiwa kupatikana hivi karibuni. Utafiti huu sio tu utawezesha kuzitambua karafuu zetu popote zitakapoonekana duniani na hivyo kusaidia katika udhibiti wa magendo ya zao hilo.

49. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa sekta ya mifugo, Serikali imeendelea kuchukua jitihada za kudhibiti magonjwa ya wanyama kwa kuimarisha huduma za chanjo. Kumekuwa na mwamko mkubwa kwa wafugaji wetu kuzitumia huduma hizo wakishirikiana na watendaji wetu walioko katika vituo vya chanjo na wale wa ugani. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya kuku 71,640, Mbwa 6,191 na Ng'ombe 1,506 wamechanjwa dhidi ya magonjwa mbalimbali yanayowaathiri wanyama hao. Sambamba na hilo, sampuli 511 zilichunguzwa maradhi mbalimbali katika maabara na sampuli 328 zilizoonekana na vimelea vya maradhi kama vile ya kuharisha damu (Coccidiosis) kwa kuku, kichaa cha mbwa (Rabies) kwa mbwa na paka, ndigana kali (East Coast Fever) na kiwele (Mastitis) kwa ng'ombe, minyoo kwa kuku, ng'ombe

na mbuzi na usugu wa vimelea vya maradhi dhidi ya dawa kwa kuku. Tunawasihi wananchi kuendelea kushirikiana na wataalamu wetu ili kuhakikisha mifugo yao inakuwa na afya bora sambamba na uzalishaji mzuri ili kupata kipato kingi na afya bora.

**Sekta ya Biashara na Viwanda**

50. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa biashara, Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kununua **tani 4,380** za karafuu kavu kwa gharama ya **Shilingi bilioni 60.4** ambapo hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya tani za Karafuu kavu **3,298.8** zimenunuliwa kutoka kwa wakulima kwa gharama ya **Shilingi bilioni 47.5** ambazo ni sawa na **asilimia 75** ya makadirio ya miezi tisa. Aidha, Serikali ilipanga kununua jumla ya **tani 786** za makonyo kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.17.** Hadi kufikia Machi, 2024 Serikali imenunua jumla ya **tani 627.6** kwa gharama ya **Shilingi milioni 941.4** sawa na **asilimia 79.8** ya makadirio. Sambamba na hayo, Serikali imeuza nje ya nchi **tani 3,190** za karafuu na **tani 694** za makonyo.

51. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendelea kuitangaza nchi yetu kibiashara imejenga kituo cha Maonesho ya Biashara huko Dimani, Wilaya ya Magharibi B. Ujenzi wa Kituo hicho kinachojumuisha ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua zaidi ya watu 1,500 na mabanda ya maonesho yenye uwezo wa kuchukua wafanyabiashara zaidi ya 650 kwa wakati mmoja hivi sasa umekamilika kwa **asilimia 80.** Hatua inayoendelea ni kumalizia ujenzi wa uwanja pamoja na ujenzi wa jengo la utawala. Ni mategemeo yetu kuwa Kituo hicho kitakuwa ni chachu kubwa katika sekta ya biashara kitaifa na kimataifa pamoja na kuvutia mikutano mikubwa ya Kikanda na Kimataifa. Aidha, Serikali itaweka utaratibu wa kutumia kumbi za mikutano zilizoko katika Kituo hicho kwa mikutano ya kitaifa itakayohusisha watu wengi kwa wakati mmoja.

52. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa maendeleo ya viwanda, hivi sasa Serikali inatekeleza Mradi wa Kuyaendeleza Maeneo Tengefu ya Biashara huko Dunga, Chamanangwe na Pangatupu. Kazi za uwekaji wa miundombinu inaendelea katika maeneo hayo ambapo eneo la Dunga ujenzi wa barabara za kiwango cha lami zenye urefu wa **kilomita 7.8** unaendelea sambamba na ujenzi wa miundombinu ya maji. Aidha, Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi (Master Plan) katika eneo la Dunga umekamilika na kwa upande Chamanangwe unaendelea. Mradi huu umelenga kuvutia uwekezaji, kutengeneza bidhaa za viwandani, kuongeza ajira kwa vijana pamoja na kuongeza mauzo ya nje.

53. **Mheshimiwa Spika,** hali ya uzalishaji katika viwanda vikubwa vilivyopo nchini inaendelea kuimarika ambapo kiwanda cha Zanzibar Milling Corporation Limited (ZMCL) kimeongeza uwezo wa kuzalisha kutoka **tani 64,800** hadi kufikia **tani 119,880** za unga wa ngano. Kiwanda cha Sukari Mahonda kimezalisha **tani 8,760** za sukari kwa mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na **tani 4,242** kwa mwaka 2022/2023. Kuimarika kwa uzalishaji wa viwanda hivi kunatoa fursa ya kuongezeka kwa ajira kwa vijana wetu ambapo Kiwanda cha Zanzibar Milling Corporation kimeajiri jumla ya wafanyakazi 200 (137 ni wa kudumu na 63 ni wa muda).

54. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuimarisha mazingira ya biashara pamoja na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda ili kusaidia kuongezeka kwa bidhaa na kukua kwa uchumi wetu. Napenda kutoa wito kwa wananchi na wafanyabiashara wote kutumia fursa zilizopo za biashara kwa lengo la kuendeleza azma ya Serikali ya kupanua wigo wa biashara pamoja na kupata ajira kupitia sekta ya viwanda na biashara.

## MASUALA MTAMBUKA

### Ajira na Uwezeshaji

55. **Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni Serikali imefanya utafiti wa taarifa za ajira kwa sekta rasmi na sekta isiyo rasmi kwa lengo la kupata takwimu za ajira na kutambua shughuli za kiuchumi na kijamii zinazofanyika hapa nchini. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa jumla ya ajira zilizozalishwa kuanzia Novemba 2020 hadi Septemba 2023 ni 187,651 sawa na asilimia 62.55 ya lengo lililowekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 ya kuzalisha ajira laki tatu (300,000) ifikapo 2025. Kati ya ajira hizo, wanaume 93,029 (49.6%) na wanawake 94,622 (50.4%). Bado Serikali inaendelea na utekelezaji wa program zake za kuzalisha ajira kwa vijana wetu ili kufikia lengo lililowekwa.

56. **Mheshimiwa Spika,** suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi ni moja ya vipaumbele vya Serikali ikiwa ni moja ya njia ya kutengeneza ajira kwa wananchi wa makundi mbalimbali. Serikali kupitia Sekta ya Uwezeshaji imeendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali ambapo jumla ya **Shilingi 7,264,764,142** zimetolewa kwa wanufaika 1,997 (wanawake 971 na wanaume 1026); Sambamba na hilo, Serikali imeunda kamati 11 za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuratibu mikopo ya Makundi Maalum ya Wajasiriamali ambapo tayari utekelezaji wa program hii unaendelea. Tunaamini mikopo hii itawasaidia wajasiriamali katika kuongeza mitaji yao na kuimarisha biashara na shughuli zao za uzalishaji.

57. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kushajihisha miradi ya maendeleo itakayotekelezwa kwa utaratibu wa Ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binasi (Public Private Pertnership - PPP). Tayari Serikali imetayarisha Muongozo wa Utekelezaji wa Miradi itakayotekelezwa kwa mfumo huo. Aidha, Serikali imekamilisha uwekaji wa kituo kitakachowasaidia wawekezaji

kuona fursa zilizopo na kurahisisha mawasiliano (PPP portal). Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024 imesajili miradi mipya 63 ya uwekezaji inayotarajia kuekeza mtaji wa Dola za Kimarekani **bilioni 1.499** na inatarajia kutoa ajira 4,392 ikilinganishwa na mwaka 2022/2023 ambapo jumla ya Miradi 62 ilisajiliwa na iliyotarajia kuekeza mtaji wa Dola za Kimarekani **milioni 540** na kutoa ajira 2,817.

**Maendeleo ya Jamii na Ustawi**

58. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na utaratibu wa kusimamia ustawi wa wazee wetu kwa kuwatunza katika makaazi maalum yaliyopo Sebleni, Welezo na Limbani. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya Wazee 69 wapo katika makaazi hayo ambapo Welezo 38 (wanawake 13 na wanaume 25), Sebleni 21 (wanawake 13 wanaume 8) na Limbani 10 (7 wanaume na 3 wanawake) na wanaendelea kupatiwa huduma za ustawi zikiwemo chakula, mavazi, malazi, matibabu na fedha za kujikimu. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha Mpango wa Pencheni ya Wazee katika jamii ambao hivi sasa una jumla ya walengwa **30,127** (Unguja 17,780 na Pemba 12,347) kati ya hao wanawake ni 17,258 na wanaume ni 12,869. Zoezi la kuwasajili wazee wanaostahiki linaendelea katika kila Wilaya. Itakumbukwa kuwa kuanzia mwaka wa fedha wa 2023/2024 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeongeza fedha za pencheni hiyo kutoka **Shilingi 20,000** hadi **Shilingi 50,000** kwa kila mzee kwa mwezi.

59. **Mheshimiwa Spika,** ni jambo la kusikitisha kuendelea kusikia juu ya kuwepo vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia katika jamii yetu. Serikali imeendelea kuchukua kila aina ya jitihada kupunguza na hatimae kuondosha kabisa vitendo hivi kwa kutoa elimu hasa kwa watoto wetu ambao mara nyingine hushawishiwa na watu hao waovu. Elimu imetolewa kwa baadhi ya Skuli na Shehia za Wilaya ya Kati na Wilaya ya Kusini Unguja na itaendelea kutolewa kwa maeneo mengine kwani ni kazi endelevu.

60. **Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine tena, naendelea kutoa wito kwa wananchi wenzangu tuendelee kushirikiana katika mapambano haya dhidi ya vitendo hivi viovu vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa rika zote.

**Sekta ya Michezo**

61. **Mheshimiwa Spika,** mbali ya kuwa ni sehemu ya burudani, michezo imekuwa ni njia moja wapo ya kuwapatia kipato vijana wetu. Aidha, michezo tumekuwa tukiitumia katika kujenga afya ya miili na akili zetu. Kwa kuthamini yote hayo, Serikali imeendelea kuimarisha na kuiendeleza sekta hii kwa kuimarisha miundombinu ya viwanja vyetu vya michezo ili kukidhi mahitaji ya makundi mbalimbali ya wanamichezo. Serikali imefanya matengenezo makubwa ya Uwanja wa Amaan (Amaan Complex) na Uwanja wa Gombani Pemba pamoja na kujenga Uwanja mpya wa kisasa Matumbaku.

62. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imepanga kujenga viwanja 16 vya michezo vya kisasa kimoja katika kila Wilaya na Mkoa ambavyo vitatumika usiku na mchana. Vile vile, Serikali imepanga kulitumia eneo la Maisara kujenga viwanja vya michezo ambavyo vitatumika kwa michezo ya aina mbalimbali. Tunaamini kuwepo kwa viwanja hivi kutasaidia kuibua vipaji zaidi vya vijana wetu katika kila aina ya michezo na hivyo kuweza kufanya vizuri kwa vilabu na timu zetu katika mashindano ya ndani na ya kimataifa.

**Udhibiti wa Dawa za Kulevya**

63. **Mheshimiwa Spika,** dawa za kulevya bado ni tatizo katika nchi yetu, ambapo suala la usafirishaji na matumizi ya dawa hizo bado limeendelea kuwa changamoto katika maeneo mengi duniani. Kwa upande wetu Serikali tunaendelea kuchukua jitihada zaidi kupambana na uingizaji na matumizi ya dawa hizo kwa watu wetu hasa vijana. Aidha, Serikali inaendelea kuhakikisha inawarejesha katika hali ya kutotumia uraibu

huo wale ambao walishaingia katika matumizi ya dawa za kulevya na kuweza kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii.

64. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekamilisha ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia huko Kidimni ambacho tayari kimeanza kutoa huduma zikiwemo za ushauri na elimu ya stadi za kazi kwa vijana walioachana na matumizi ya dawa za kulevya. Jumla ya vijana 124 wamepatiwa huduma hiyo na vijana 18 kati yao wamefanikiwa kuachana kabisa na matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, Serikali imewaunganisha tena na jamii waraibu waliopata nafuu ili waweze kuendelea na shughuli zao za kuendesha maisha.

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine Serikali inaendelea na operesheni za kuwasaka watu wanaojihusisha na biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika maeneo yote mijini na mashamba. Katika kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai, 2023 jumla ya watuhumiwa 158 (144 wanaume, na 14 wanawake) Unguja na Pemba walishikwa wakihusishwa na kesi za dawa za kulevya za aina mbalimbali. Serikali itaendelea kupambana na wote ambao kwa njia moja au nyengine watabainika kujihusisha na dawa hizo kwa njia yeyote. Tunaendelea kuwaomba na kuwasisitiza wananchi kutoa ushirikiano kwa watendaji wa mamlaka zinazohusika na mapambano haya pindi wanapobaini viashiria vya kufanyika biashara hizi katika maeneo yao.

66. **Mheshimiwa Spika,** maelezo haya juu ya masuala mbalimbali ya kisekta nimeyaeleza kwa muhutasari tu kwa baadhi ya sekta, maelezo ya ndani zaidi yatatolewa na Waheshimiwa Mawaziri wa sekta husika wakati watakapowasilisha hotuba zao za bajeti.

67. **Mheshimiwa Spika,** sasa kwa ridhaa yako naomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 na malengo ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI – MACHI 2023/2024)**

68. **Mheshimiwa Spika,** kazi za kawaida na miradi ya maendeleo kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, zinatekelezwa kupitia Idara saba na Taasisi tatu. Kutokana na utaratibu wa Serikali wa kutekeleza majukumu yake kwa kutumia Bajeti inayotumia Programu (Programme Based Budget), Ofisi kupitia Idara na Taasisi hizo inatekeleza Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14. Aidha, Programu hizo zinatekelezwa kupitia Mafungu matatu ya kibajeti ambayo ni:

i C01 – Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

ii C02 – Baraza la Wawakilishi, na

iii C03 – Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar

69. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Machi 2023/2024, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Program zake imetekeleza kazi za kawaida na kazi za miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:

**C01 – OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

**PROGRAMU KUU - C0101: URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

**Programu Ndogo - (C010101): Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais**

70. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo moja ya Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais ambayo jukumu lake ni kuratibu kazi za kila siku za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais pamoja na utoaji wa huduma zote muhimu

anazostahiki Makamu wa Pili wa Rais. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeratibu ziara 18 za ndani ya nchi (Unguja, Pemba na Tanzania Bara) za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi na miradi ya Serikali katika maeneo mbalimbali;

ii. Imeratibu jumla ya Mikutano 34 baina ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na wageni mbali mbali wakiwemo watendaji wa Serikali, Wawekezaji na Wageni Mashuhuri;

iii. Imepokea malalamiko na migogoro 97 kutoka kwa wananchi inayohusu Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Ofisi imeratibu na kuwasilisha malalamiko na migogoro yote kwa Taasisi husika ili kupatiwa ufumbuzi. Ofisi inaendelea kufuatilia maendeleo ya utatuzi huo kwenye taasisi zinazoshughulikia;

iv. Ofisi imeendelea kutoa taarifa juu ya shughuli na matukio 45 aliyoyafanya au kushiriki Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, imehifadhi hotuba 39 na picha 545 zinazohusiana na shughuli alizofanya au kushiriki Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya kumbukumbu na matumizi ya baadae;

v. Imeratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi alizozitoa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa wananchi, taasisi na jamii zinazolenga kuleta maendeleo;

**71.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii inayotekelezwa na Afisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,631,251,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia

Machi, 2024 imetumia **Shilingi 1,040,456,353** ambazo ni sawa na **asilimia 83** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 64** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

**PROGRAMU KUU - (CO102): URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI**

72. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu ina jukumu la kuweka mfumo imara na endelevu wa utoaji na upatikanaji wa huduma bora za Serikali kwa jamii. Programu hii ina Programu Ndogo nne ambazo ni Kukabiliana na Maafa, Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shughuli za SMZ – Dodoma. Maelezo ya utekelezaji wa kazi kwa kila Programu Ndogo ni kama ifuatavyo:

**Programu Ndogo – (CO10201): Kukabiliana na Maafa**

73. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa ina jukumu la kuainisha, kuimarisha na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Kukabiliana na Maafa hapa Zanzibar ambayo inalenga kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa. Katika kipindi cha Julai – Machi cha mwaka wa fedha 2023/2024, Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeratibu operesheni na utoaji wa huduma na misaada ya kibinaadamu katika matukio 92 ya majanga/maafa yaliyotokea Unguja na Pemba yakiwemo matukio 15 ya upepo mkali, matukio 68 ya moto, matukio manne (4) ya ajali za baharini na tukio moja la mafuriko kutokana na mvua za Vuli zilizonyesha mwezi Novemba 2023. Aidha, tukio la kula kasa anaesadikiwa kuwa na sumu katika eneo la Kisiwa Panza Mkoani Pemba ambapo watu 167 waliathirika ambapo watu tisa (9) kati yao walipoteza

maisha. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awajaalie malazi pema peponi - Amin;

ii. Imetoa mafunzo ya kukabiliana na maafa kwa waendesha boda boda 95 kati yao 45 kutoka wa Wilaya ya Magharibi “A” na 50 wa Wilaya ya Kaskazini “A”. Mafunzo hayo yalijikita katika tahadhari juu ya kujikinga na ajali za barabani ambazo zimekuwa zikipoteza nguvu kazi kubwa ya vijana na jamii kwa jumla. Elimu ya kukabiliana na maafa pia imetolewa kwa Kamati za Kukabiliana na Maafa sita (6) za Wilaya ya Kati na Kamati zote nne za Wilaya ndogo Tumbatu;

iii. Imetoa taarifa za tahadhari za mapema juu ya muelekeo wa mvua za Vuli za mwaka 2023 na mvua za Masika za mwaka 2024 na athari zinazoweza kujitokeza kwa njia mbalimbali ikiwemo kufanya vikao na wadau wa maafa, wenyeviti wa Kamati za Kukabiliana na Maafa za Wilaya na Shehia za Unguja na Pemba ili kuchukua tahadhari za mapema kabla ya mvua hizo hazijanyesha;

iv. Imerusha hewani jumla ya matangazo manne (4) ya tahadhari na vipindi 12 (ZBC TV (3) na ZBC Radio (6), Bahari FM (1) na Zanzibar Cable (1) na Radio Jamii Tumbatu (1) pamoja na kutuma ujumbe wa pamoja (Bulk sms) kwa jamii ili kuchukua hatua stahiki katika kujikinga na majanga mbali mbali yanayoweza kutokea;

v. Ofisi kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika, imefanya kaguzi 22 Unguja na Pemba katika taasisi mbali mbali za Serikali na zisizo za Kiserikali na maeneo hatarishi ili kubaini uzingatiaji wa miongozo ya kukabiliana na maafa katika maeneo hayo. Miongoni mwa taasisi na maeneo yaliyofanyiwa kaguzi ni Hoteli ya Ocean view, Chuo cha Utalii Maruhubi, vyombo vya usafiri vya abiria katika visiwa vya Makoongwe na Kisiwa panza na vyoo katika Skuli ya Fidel Castro na Mabaoni. Timu

ya ukaguzi ilibaini uwepo wa baadhi ya changamoto zikiwemo za utunzaji hafifu wa mazingira na ukosefu wa baadhi ya miundombinu ya kukabiliana na maafa. Baada ya kaguzi hizo na maelekezo yaliyotolewa, tayari hatua zimechukuliwa ikiwemo kubomoa kuta zilizoziba njia za maji na misingi na maboma yaliyopo katika maeneo hatarishi yenye kutuama maji;

vi. Ofisi imeziimarisha ghala za kuhifadhia vifaa vya misaada ya kibinadamu kwa kununua vifaa mbali mbali yakiwemo mahema, vyandarua, magodoro, mabusati, bati na makoti ya uokozi (life jackets) ambayo yatatumika wakati wa dharura kama itakavyoelekezwa;

vii. Imeratibu na kufanya ziara katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuangalia shughuli za kukabiliana na maafa. Miongoni mwa maeneo hayo ni Kituo cha Uokozi kiliopo Mkoani Pemba, redio za mawasiliano ya dharura, Kiwanja cha Ofisi za Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kiliopo Mgogoni, na Kituo cha Zimamoto na Uokozi (KZU) Chanjaani Pemba pamoja na kutembelea Kituo cha Uokozi kinachosimamiwa na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) na kituo cha mawasiliano ya dharura (call center).

viii. Imefanya Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kukabiliana na Maafa ambayo hufanyika kila ifikapo tarehe 13 Oktoba ya kila mwaka. Miongoni mwa shughuli zilizofanyika katika maadhimisho haya ni kukabidhi vifaa vya uokozi na misaada ya kibinadamu kwa kamati za uvuvi Jambiani na vikosi vya uokozi (KMKM na KZU), kushajihisha mazoezi ya kuzuia kuzama kwa wanafunzi wa skuli za msingi na sekondari. Aidha, kilele cha maadhimisho ya siku hiyo kilifanyika katika Ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdul Wakil - Kikwajuni ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar;

ix. Imeandaa na kuendesha zoezi la kujiandaa na kujiweka tayari kukabiliana na maafa pamoja na kupima uwezo wa taasisi na jamii katika kukabiliana na majanga ya aina mbalimbali (simulation exercise);

x. Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Timu ya Afya ya Wilaya (DHMT) imefanya mkutano na wajumbe wa Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya ya Mkoani, vitengo vyote vya Wizara ya Afya, na wadau wengine wa sekta mbali mbali kwa ajili ya kuandaa mikakati na hatua zinazofaa kuchukuliwa katika kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mvua zinazotarajiwa kunyesha;

xi. Imeratibu na kusimamia uchimbaji na ujenzi wa msingi wa kupitisha maji ya mvua katika eneo la Kibonde Mzungu ambao utasaidia kuondosha/kupunguza changamoto ya kujaa maji katika makaazi ya wananchi wanaoishi karibu na eneo hilo. Msingi huo una urefu wa **mita 345** na umegharimu jumla ya **Shilingi 441,407,030;**

xii. Imefanya kikao cha kupokea maoni ya Mapitio ya Mpango Mkakati wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa wa mwaka 2024 – 2028 pamoja na kuendelea kuifanyia mapitio Sera ya Kukabiliana na Maafa ya Mwaka 2011;

xiii. Imeendelea kutoa mafunzo kwa watendaji wake ikiwemo mafunzo ya muda mrefu kwa mfanyakazi mmoja anayesomea ngazi ya shahada ya uzamili fani ya masuala ya mabadiliko ya tabia nchi na maafa na wafanyakazi watatu wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi;

**74. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii Ndogo inayotekelezwa na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,581,510,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2024 imetumia **Shilingi 983,354,315** ambazo ni

sawa na **asilimia 82** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 62** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

### Programu Ndogo – (CO10202): Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa

**75. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo yenye jukumu la kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na shughuli za kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa inatekelezwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024) imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeratibu Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambazo kilele chake kilifanyika Uwanja wa Amaan na Mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, jumla ya miradi 64 ya Maendeleo ilizinduliwa na miradi 45 iliwekewa mawe ya msingi katika maadhimisho hayo;

ii. Imeshiriki na kuratibu ushiriki wa Viongozi kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Maadhimisho ya Siku ya Mashujaa yaliyofanyika katika Viwanja vya Mji wa Serikali Dodoma siku ya tarehe 24 Julai, 2023;

iii. Imeratibu na kushiriki katika mazishi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mstaafu Hayati Edward Ngoyai Lowasa yaliyofanyika kuanzia Tarehe 10 Februari, 2024 na kuzikwa tarehe 17 Februari, 2024 nyumbani kwake Kijijini Ngarashi, Wilaya ya Monduli, Mkoa wa Arusha;

iv. Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu imeratibu Mazishi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mstaafu Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi yaliyofanyika

Tarehe 2 Machi, 2024 – Mangapwani, Wilaya ya Kaskzini B, Mkoa wa Kaskazini Unguja. Aidha, Ofisi imeratibu Hitma mbili za Hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi zilizofanyika tarehe 3 Machi, 2024 katika Viwanja vya Nyamanzi na tarehe 5 Machi, 2024 katika Msikiti wa Jamii Zinjibar, Mazizini;

v. Imeshiriki katika vikao vya maandalizi ya Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambazo kilele chake kilifanyika tarehe 26 Aprili, 2024 Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam;

vi. Imeratibu maadhimisho ya Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa na Siku ya Kumbukumbu ya Karume ambayo yalianza tarehe 1 Aprili, 2024 na kukamilika tarehe 7 Aprili, 2024. Maadhimisho hayo yalianza kwa ziara na dua katika makaburi yote ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Waasisi wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar pamoja na kaburi la aliyekuwa Katibu wa Kwanza wa Chama Cha Afro Shirazi na kukamilika kwa dua maalum ya kumuombea Mzee Abeid Amani Karume na Viongozi wengine waliotangulia mbele ya haki iliyofanyika Afisi Kuu ya Chama cha Mapinduzi, Kisiwandui, Zanzibar;

vii. Imefanya matengenezo makubwa ya jengo la ofisi la Mwanakwerekwe yaliyohusisha ujenzi wa ukuta (fensi) na kufanya ukarabati mkubwa wa ghala la kuhifadhia vifaa vya sherehe liliopo katika Ofisi zake Mwanakwerekwe;

viii. Ofisi imenunua vifaa mbalimbali vya kisasa kwa ajili ya maadhimisho na sherehe za kitaifa vikiwemo mashamiana, vifaa vya mitambo ya sauti (PA System), majukwaa makubwa na kamera;

ix. Imeendelea kutoa huduma za ukodishaji wa maduka yaliyopo Mwanakwerekwe pamoja na kukodisha vifaa vya sherehe.

76. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii Ndogo inayotekelezwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,683,357,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2024 imetumia **Shilingi 2,252,123,244** ambazo ni sawa na **asilimia 143** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 134** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

77. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii Ndogo vilevile inahusika na ukusanyaji wa mapato kutokana na ukodishaji wa maduka na vifaa vya sherehe. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, Idara ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 52,710,000** na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024 Idara imekusanya jumla ya **Shilingi 22,405,600** ambayo ni sawa na **asilimia 52** kwa fedha iliyotengwa miezi tisa na **asilimia 43** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

**Programu Ndogo – (SCO10203): Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

78. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina jukumu la kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, masuala ya Muungano, ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, Utafiti kitaifa pamoja na kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) hapa Zanzibar. Programu hii ndogo ambayo inatekelezwa na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024), imetekeleza yafuatayo:

    i. Imeratibu na kusimamia upatikanaji wa vibali vya utafiti ambapo jumla ya vibali 439 vilitolewa kwa watafiti wa ndani na nje ya nchi ikijumuisha Taasisi 33 (Taasisi 18 za Serikali na Taasisi 15 za Binafsi), wageni walikuwa ni 41 na Wenyeji ni 355;

ii. Imefanya vikao vya maandalizi ya uandaaji wa mfumo wa mtandao wa maombi ya Utafiti Zanzibar kwa kushirikiana na Tume ya Kitaifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Mfumo huo utawawezesha Watafiti kuomba vibali na kupata kwa njia ya Mtandao;

iii. Imeshiriki Kikao cha Kamati ya Kitaifa cha Utoaji wa vibali Tanzania kilichofanyika tarehe 28/02/2024 katika ukumbi wa COSTECH Dar es Salaam. Kikao hicho kilipitia maombi mbali mbali ya utafiti pamoja na kujadiliana kuhusu mapitio ya Miongozo ya Utoaji wa vibali vya utafiti kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar;

iv. Imeratibu na kuandaa vikao vya pamoja vilivyohusisha Idara ya Uhamiaji Zanzibar, Afisi ya Rais – Kazi, Uchumi na Uwekezaji (Kazi na Uwezeshaji), Wakala Binafsi wa Ajira na Wawakilishi wa Mashirika ya ndege kujadili changamoto zinazowapata watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi. Vikao hivyo vilivyofanyika katika Ukumbi wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Vuga Zanzibar na katika Ukumbi mdogo wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar;

v. Imeratibu na kusimamia uingizwaji wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa mwaka 2023/2024 ambapo hadi sasa majimbo 41 yameshapokea fedha **Shilingi 820,000,000** za miradi ya Mfuko huo ambazo ni sawa na **Shilingi 20,000,000** kwa kila jimbo. Vilevile imefanya ziara ya mafunzo nchini Zambia kwa ajili ya kuimarisha usimamizi na uratibu wa uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hapa Zanzibar;

vi. Imefanya ufuatiliaji na kutoa mafunzo ya utekelezaji wa Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo 18 ya Pemba kwa mwaka wa Fedha 2022/2023. Ufuatiliaji huo umebaini kasoro mbalimbali zilizojitokeza kupitia

marejesho yaliyowasilishwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Unguja na Pemba. Kupitia kasoro hizo, wajumbe wa kamati za Majimbo 17 za Pemba wamejengewa uwezo ili kutekeleza majukumu yao kwa kufuata sheria na taratibu za manunuzi sambamba na sheria nambari 4 ya mwaka 2012 na marekebisho yake ya mwaka 2016;

vii. Imeratibu, kuandaa na kuwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Miaka mitatu (2020 – 2023). Taarifa hiyo imeandaliwa kwa pamoja baina ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - SMZ na Ofisi ya Waziri Mkuu – SJMT na kuwasilishwa kwa Mamlaka husika;

viii. Imeendelea kuratibu mpango mpito wa Jamii ni Afya unaotekelezwa na D-tree International kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ili kusaidia utekelezaji wa mpango kusimamiwa na Serikali. Aidha, jumla ya vikao kazi vinne (4) vimefanyika Unguja na Pemba. Vikao hivyo ni:

a. Uzinduzi wa Kamati Maalum (Steering Committee) ya Mpango wa Jamii ni Afya itakayosimamia utekelezaji wa mpango huo,

b. Utambulisho wa Mpango wa Jamii ni Afya na njia za kuwatumia Wahudumu wa Jamii ni Afya (CHW) kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto,

c. Kikao kazi cha kutambulisha Mpango wa Jamii ni Afya kwa Wakuu wa Wizara na Taasisi za Serikali zilizopo Pemba,

d. Kikao cha kujadili Mpango Mpito wa Jamii ni Afya (Jamii ni Afya Transition Plan 2023-2024) kwa Wajumbe wa kamati mbili za kudumu za Baraza la Wawakilishi (Kamati ya Ustawi wa Jamii na Kamati ya Bajeti),

ix. Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais - SJMT imeandaa na kutoa mafunzo ya uendeshaji na utekelezaji wa Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Sura 96 ya mwaka 2009. Kikao kazi hicho ambacho kiliwashirikisha Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar na watendaji wa Halmashauri/Manispaa za Zanzibar. Vile vile kilifuatilia ufungaji hesabu za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo wa Mbunge (CDCF) uliofanyika kwa majimbo yote ya Zanzibar;

x. Imefanya ufuatiliaji wa usaili wa vijana walioomba nafasi za ajira za Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji kwa upande wa Zanzibar ambao ulienda vizuri;

xi. Imeandaa na kushiriki katika kikao cha Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia masuala ya Muungano kilichofanyika Zanzibar tarehe 21 Agosti, 2023. Sekretarieti hiyo ilifanya maandalizi ya kikao cha Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ cha kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 22 Septemba, 2023;

xii. Imeratibu na kushiriki kikao cha Mawaziri wa SJMT na SMZ cha kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Zanzibar tarehe 05 Machi, 2024 na Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano kilichofanyika tarehe 06 Machi, 2024 Zanzibar. Vikao hivyo, vimeagiza kuendelea kufanyiwa kazi kwa Hoja za Muungano zilizopo;

xiii. Imeratibu na kushiriki vikao vitano (5) vya mashirikiano baina ya Wizara/Sekta za SMZ na SJMT vifuatavyo:

    a. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kikao kilichofanyika Dar es Salaam kuanzia tarehe 26 - 27 Oktoba 2023;

b. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Ofisi ya Waziri Mkuu, kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 18 Novemba 2023;

c. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (SMZ) na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (SJMT) kilichofanyika Zanzibar tarehe 23 Novemba, 2023;

d. Sekta ya Utalii (SMZ) na Sekta ya Utalii (SJMT) kilichofanyika Pemba kuanzia tarehe 28 Januari hadi 03 Februari, 2024; na

e. Sekta ya Uchukuzi (SMZ) na Sekta ya Uchukuzi (SJMT) kilichofanyika Tanga kuanzia tarehe 6 - 8 Februari, 2024 na kujadili changamoto za bandari baina ya Zanzibar, Dar es Salaam na Tanga.

xiv. Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (SJMT) imeratibu na kushiriki katika mafunzo ya utayarishaji wa ufungaji hesabu kwa wahasibu wa Manispaa/Mabaraza ya Miji na Halmashauri wanaoshughulikia Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF) kwa upande wa Pemba kuanzia tarehe 13 - 5 Disemba, 2023. Vilevile Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (SJMT), Ofisi imefanya uhakiki wa Hoja za Wakaguzi kuhusu Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo wa Mbunge kwa Majimbo yote ya Zanzibar kuanzia tarehe 19 – 27 Disemba, 2023;

xv. Imefanya ufuatiliaji katika Taasisi zenye hoja za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi kuanzia tarehe 18 - 29 Disemba, 2023. Tathmini ya Utekelezaji wa Hoja hizo inaendelea kufanyiwa kazi;

xvi. Imeratibu na kuashiriki katika kazi ya kuandaa Kitabu cha Miaka 60 ya Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambacho kinalenga kutoa

elimu kwa umma kuhusu muundo, majukumu, viongozi waliohudumu na mafanikio na changamoto za Ofisi hiyo.

xvii. Imeshiriki katika kikao Maalum cha Kamati ya Usimamizi wa Programu ya Kuendeleza Kilimo na Mifugo (AFDP) kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Waziri Mkuu – Magogoni – Dar es Salaam. Kikao hicho kilifuatiwa na Kikao cha Mawaziri ambacho kilipitia na kutoa muelekeo wa maazimio ya moja ya shughuli za mradi huo kuhusu ununuzi wa meli nane za uvuvi wa bahari kuu zitakazotumika Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, kikao chengine cha Kamati ya Ushauri wa kiufundi (ITAC) kilifanyika Dar es Salaam tarehe 05 Septemba, 2023;

xviii. Imeratibu na kushiriki katika tathmini ya utekelezaji wa miradi mitano ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayotekelezwa Zanzibar. Miradi hiyo ni Ujenzi wa Nyumba 3 za makaazi ya Askari Tunguu (asilimia 40); Ujenzi wa Nyumba 4 za askari Makunduchi (asilimia 20); Ujenzi wa Kituo cha Polisi cha kisasa Makunduchi (asilimia 96), Ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Kisasa Tumbatu (asilimia 65), Ujenzi wa Maktaba ya Polisi, Ziwani (asilimia 80);

xix. Imeratibu na kushiriki vikao 4 vya Mikutano ya Baraza la Wawakilishi ambayo ni mkutano wa Kumi na Moja wa Baraza la Kumi la Wawakilishi uliojadili Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka wa Fedha 2023/2024, Mkutano wa Kumi na Mbili wa Baraza la Kumi la Wawakilishi ulioanza tarehe 13-09-2023 hadi 14/10/2023, Mkutano wa Kumi na Tatu wa Baraza la Kumi la Wawakilishi ulioanza tarehe tarehe 29-11-2023 hadi 08/12/2023 na Mkutano wa Kumi na Nne wa Baraza la Kumi la Wawakilishi ulioanza tarehe 14/02/2024 hadi 01/03/2024,

xx. Imeshiriki vikao Maalum vya Baraza la Vyama vya Siasa kikiwemo cha majadiliano ya hali ya vyama vya siasa kutumia viongozi wa dini katika shughuli za siasa nchini, mavazi na vitendo vya walinzi wa viongozi wa vyama vya siasa na lugha zinazotumika katika mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa nchini kilichofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 01/08/2023 na Kikao cha kutathmini Utekelezaji wa Mapendekezo ya Vikosi kazi vilivyoundwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kujadili hali ya siasa nchini kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 11-13/09/2023;

xxi. Imefanya vikao kwa wadau wa Siasa Zanzibar, ikihusisha Vyama vya Siasa (15) na Taasisi za Serikali sita (6) kwa lengo la kuandaa ripoti na kufanya tathmini ya hali ya siasa Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitatu;

xxii. Imetoa mafunzo ya Muongozo wa Uandaaji na Uandishi wa Sera za Kisekta – Zanzibar 2022 kwa Maafisa wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Tume ya Mipango Zanzibar ili kusaidia kufanya maboresho ya Sera za Tume ya Mipango watakazozitayarisha ili kuendana na Muongozo uliopo sasa. Aidha, mafunzo hayo yalitolewa kwa Maafisa Wadhamini wa Wizara zote huko Pemba sambamba na kuwapatia vitabu vya Muongozo huo;

xxiii. Imefanya ziara za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera za Kisekta nchini kwa Mawizara na Taasisi za Serikali ikiwa na lengo la kupima utekelezaji za Sera kwa kipindi cha miaka mitatu;

xxiv. Imeratibu na kusimamia shughuli za Idara ya Uhamiaji Zanzibar.

79. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi inasimamia na kutekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF) Zanzibar ambao ni

Mpango wa Kitaifa unaotekelezwa Tanzania Bara na hapa Zanzibar. Lengo la Mpango huu ni kuziwezesha kaya masikini sana kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji ya msingi hasa upatikanaji wa uhakika wa chakula na huduma muhimu za afya na elimu kwa watoto wa kaya za walengwa kwa lengo la kutengeneza rasilimali watu ya baadae.

80. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango huu, unahusisha maeneo mawili ya utekelezaji kwa Unguja na Pemba ambapo jumla ya Kaya **54,133** (Unguja **25,264** na Pemba **28,869**) zinanufaika. Mpango huu unakwenda sambamba na mipango ya Serikali zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuzingatia vipengele muhimu vya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 – 2050, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, Mpango Maendeleo Zanzibar 2021 – 2026 (ZADEP) pamoja na maelekezo ya hotuba mbali mbali za viongozi wetu Wakuu wa Nchi. Utekelezaji wa Mpango huu katika vipengele vyake vyote ni kama ifuatavyo:

i. Ofisi kupitia Mpango huu imeendelea kuratibu shughuli za uhaulishaji wa fedha kwa kaya za Walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kwa vipindi vya malipo vya March – Aprili, Mei – Juni, Julai – Agosti, na Septemba – Oktoba, 2023 ambapo jumla ya Shilingi 4,577,236,746 zimelipwa kwa kaya 24,206 kati ya kaya 24,491 sawa na asilimia 99.61 na kaya 285 hazikuonekana katika vituo vya malipo kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo kufariki kwa mhusika wa kaya pamoja na kutohudhuria katika siku za malipo. Aidha, kati ya fedha zilizolipwa, jumla ya Shilingi 208,259,000 zimelipwa kwa kaya 1,240 kwa shehia 18 za tathmini ya Mpango – (Impact Evaluation Shehia) ikiwa ni malipo ya Awamu ya Pili ya Ruzuku ya Uzalishaji (Second Installment of Productive Grants) kwa kaya hizo;

ii. Ofisi imeendelea na usimamizi wa utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu (Targeted Infrastructures) miradi sita ya ujenzi imetekelezwa na miradi miwili miongoni mwao tayari imekamilika. Miradi hiyo ni Ukarabati wa Majengo ya Skuli ya Kizimkazi Mkunguni, Ujenzi wa Jengo la Wazazi (Maternity Ward), Donge Pwani, Ujenzi wa Kituo cha Afya Daraja la Pili , Uzi Ng'ambwa, Ujenzi wa Ukumbi wa Mitihani Skuli ya Bambi, Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Upenja na Ujenzi wa Kituo cha Afya Daraja la Pili, Kinyikani. Hali ya Utekelezaji wa miradi hiyo inaonekana katika Kiambatisho Nam. 1;

iii. Ofisi imeendelea uratibu wa utekelezaji wa Uhaulishaji Fedha kwa Walengwa wa Mpango (Conditional Cash Transfer) ambapo hivi sasa asilimia 99 ya Watoto wa Walengwa wameweza kutimiza masharti ya Elimu na Afya hivyo kuziwezesha kaya husika kupata ruzuku zinazohusiana na masharti ya elimu na afya. Katika kuimarisha utoaji wa huduma hii kwa walengwa, Ofisi iliendesha mafunzo ya siku sita juu ya usimamizi wa fomu za Masharti ya Elimu na Afya kwa Walimu na Wauguzi wa afya ambapo jumla ya washiriki walikuwa 753 (Walimu 649 na Wauguzi 104);

iv. Ofisi imeratibu zoezi la usajili wa vikundi vya Kuweka na Kukuza Uchumi wa Kaya lilotekelezwa na Maafisa ushirika Wilaya ambapo kwa Unguja jumla ya vikundi 389 vilisajiliwa. Mchanganuo wa idadi Kiwilaya unaonekana Kiambatisho Nam. 2;

v. Vilevile, Ofisi imesimamia muendelezo wa utoaji wa Ruzuku za Uzalishaji (Productive grants) kwa kaya maskini ambapo jumla ya Shilingi 569,706,140 zimelipwa kwa kaya 2,918.

81. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Mpango huu Ofisi iliratibu ziara ya kimafunzo kwa Kamati ya Usimamizi wa Mradi Shehia ya Kizimkazi Mkunguni katika Mkoa wa Geita, Halmashauri ya Wilaya ya Chato. Ziara hiyo ilianza tarehe 19 hadi 24 Septemba, 2023 kwa kutembelea miradi iliyotekelezwa pamoja na kufanya majadiliano na wasimamizi wa miradi iliyotembelewa;

82. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii Ndogo inayotekelezwa na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 925,969,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2024 imetumia **Shilingi 644,936,860** ambazo ni sawa na **asilimia 93** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 70** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

83. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii Ndogo kupitia Programu ya TASAF pia ilipangiwa **Shilingi 17,646,457,000** kwa kazi za maendeleo ambapo **Shilingi 17,546,457,000.** ni mchango wa Washirika wa Maendeleo na **Shilingi 100,000,000** ni mchango wa Serikali. Hadi kufikia Machi 2024 ilipata jumla ya **Shilingi 9,323,768,246** ambazo ni sawa na asilimia 53 ambapo **Shilingi 9,298,768,246** ni mchango wa Washirika wa Maendeleo sawa na **asilimia 53** na **Shilingi 25,000,000** ni mchango wa Serikali sawa na **asilimia 25** zilizopangwa kwa mwaka.

84. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Baraza hili liliidhinisha matumizi ya **Shilingi 18,499,900,000** ikiwa ni ruzuku kwa Idara ya Uhamiaji, Zanzibar na hadi Machi 2024 ilipata **Shilingi 12,333,264,333** ambazo ni sawa na **asilimia 89** kwa fedha zilizotengwa miezi tisa na **asilimia 67** kwa fedha zilizopangwa kwa mwaka.

## Programu Ndogo – (CO10204): Shughuli za SMZ – Dodoma

**85. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Shughuli za SMZ, Dodoma jukumu lake kuu ni kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Tanzania Bara kwa lengo la kurahisisha mipango na utekelezaji wa shughuli za SMZ huko Tanzania Bara pamoja na kukuza na kuimarisha ushirikiano baina SMZ na Serikali na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Washirika wa Maendeleo, Taasisi za Kimataifa na Ofisi za Kibalozi. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeratibu na kushiriki vikao 28 vya mashirikiano ya kazi baina ya Wizara za SMZ, SJMT, Ofisi za Kibalozi, Taasisi na Jumuiya za Kimataifa (Kiambatisho Nam. 3);

ii. Imeratibu na kutoa huduma ya usafiri kwa Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanapofanya ziara na kuhudhuria mikutano Dar es Salaam na Mikoa mingine Tanazania Bara pamoja na kuratibu upatikanaji VISA 29 kwa Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanawaotarajia kusafiri nje ya nchi;

iii. Imeandaa mafunzo ya masuala mtabumbuka kwa wafanyakazi 33 wa Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma;

**86. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii Ndogo inayotekelezwa na Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dodoma iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 976,659,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2024 imetumia **Shilingi 511,623,458** ambazo ni sawa na **asilimia 68** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 52** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

**GRAMU KUU – CO104: UENDESHAJI NA URATIBU WA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

87. **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu hii ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inahusika na uimarishaji wa mazingira bora ya wafanyakazi na usimamizi wa mipango na shughuli za kiofisi. Programu hii ina Programu Ndogo tatu (3) ambazo ni Uongozi na Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi Kuu Pemba.

**Programu Ndogo – (CO10401): Uongozi na Utawala**

88. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii Ndogo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na inahusika na usimamizi wa rasilimali za ofisi na utekelezaji wa kazi za kila siku za Ofisi. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ndogo hii imetekeleza yafuatayo:-

i. Imesimamia maslahi na stahiki za wafanyakazi wa Ofisi zikiwemo za mishahara, michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na Mfuko wa Bima ya Afya (ZHSF), likizo pamoja na stahiki nyenginezo;

ii. Imeratibu na kusimamia utoaji wa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 36 wa Idara na Taasisi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika fani na ngazi mbali mbali ndani na nje ya nchi. (Kiambatisho Nam. 4). Vile vile imeratibu na kusimamia utoaji wa mafunzo ya wastaafu kwa wafanyakazi 3 wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) kwa lengo la kujenga uelewa juu ya maisha baada ya kustaafu kazi;

iii. Imesimamia shughuli za uendeshaji ikiwemo ununuzi wa vitendea kazi pamoja na kulipia gharama za umeme, mawasiliano ya simu na vyombo vya usafiri. Aidha,

Idara imefanya ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ikiwemo upakaji wa rangi, usawazishaji wa mkingo (gata) za kupokea maji ya mvua na uzibuaji wa mfumo wa maji taka kupitia Baraza la Manispaa Mjini.

iv. Imeimarisha miundombinu ya upatikanaji wa huduma za maji kuweka mashine ya maji (pressure pump) na mashine ya kupandisha maji katika jengo la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Vuga pamoja kuimarisha miundombinu ya umeme kwa kuweka "phase balance" ambayo imeweza kusaidia kupunguza changamoto ya upatikanaji wa umeme mdogo kwa baadhi ya maeneo ya jengo;

v. Ofisi imeimarisha mifumo ya TEHAMA kwa ufungaji wa "network" mpya katika jengo la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Vuga kwa lengo la kurahisisha utendaji kazi wa Ofisi;

vi. Imeendesha vikao vitatu vya kawaida vya Kamati ya Uongozi, vikao vitatu vya Kamati Tendaji na vikao viwili vya Bodi ya Zabuni kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi;

vii. Imetoa huduma za mikutano 76 katika Ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul Wakil ambayo ilishirikisha Viongozi na watendaji wa ngazi mbalimbali wa Serikali.

**89. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii Ndogo inayotekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliidhinishiwa **Shilingi 1,592,483,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2024 imetumia **Shilingi 1,034,180,458** ambazo ni sawa na **asilimia 86** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 65** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

## Programu Ndogo – (CO10402): Mipango, Sera na Utafiti

**90. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ambayo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inahusika na uratibu wa masuala ya bajeti, uibuaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na masuala ya sera na tafiti zinazohusu masuala yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2023/2024 programu ndogo hii imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeandaa Mpango kazi na Mpango wa Utekelezaji wa Ofisi wa mwaka 2023/2024, Taarifa ya utekelezaji wa Robo ya kwanza, Nusu Mwaka na Taarifa ya Utekelezaji ya Miezi Tisa 2023/2024 pamoja na kuandaa bajeti ya mwaka 2024/2025.

ii. Imefanya ziara za ufuatiliaji na tathmini kwa miradi na shughuli zinazosimamiwa na Ofisi pamoja na kuandaa taarifa za ufuatiliaji na tathmini za mwezi, robo mwaka na miezi tisa kwa mwaka 2023/2024 na kuziwasilisha Tume ya Mipango;

iii. Imeandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Ofisi kwa vipindi vya Robo mwaka 2023/2024 na taarifa nyengine za kiutendaji na kuziwasilisha katika mamlaka mbalimbali ikiwemo Tume ya Mipango na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi;

iv. Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango imefanya mafunzo kwa Maafisa Mipango wanaohusiana na Bajeti kwa ajili ya matayarisho ya Bajeti ya mwaka fedha 2024/2025;

v. Imeratibu na kushiriki katika utafiti wa maandalizi ya uandaaji wa Sera ya Usalama wa Raia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande Zanzibar;

vi. Inaendelea kuratibu na kushiriki katika kuifanyia mapitio Sera ya Kukabiliana na Maafa ya Mwaka 2011;

vii. Imeandaa na kuendesha vikao vya mashrikiano baina ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na pia baina ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Ofisi ya Waziri Mkuu ambavyo vilifanyika Dar es Salaam;

viii. Ofisi imeendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli za Kitengo cha Uratibu na Usimamizi wa Kitaifa wa Mfuko wa Fedha wa Dunia (ZGFCCM) kwa kufuatilia shughuli zote zinazofanywa na Programu za Kukabiliana na Maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria katika maeneo ya miradi kwa Unguja na Pemba.

91. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 442,690,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2024 imetumia **Shilingi 256,480,875** ambazo ni sawa na **asilimia 74** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 58** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

**Programu Ndogo – (CO10403): Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi – Pemba**

92. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inatekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba. Kwa vile shughuli zinazofanywa na Idara na Taasisi za Ofisi Unguja vilevile hutekelezwa Pemba, Programu hii inahusika zaidi na uratibu wa shughuli hizo kwa upande wa Pemba sambamba na shughuli za kiutawala za kila siku. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2023/2024. Programu ndogo hii imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeratibu jumla ya ziara sita (6) za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais alizofanya kisiwani Pemba;

ii. Imeendelea kuimarisha mazingira mazuri ya kufanyia kazi na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ikiwemo maslahi na mafunzo ya watumishi, matengenezo ya majengo pamoja na ununuzi wa huduma na vifaa vya kufanyia kazi;

iii. Imeandaa Mipango ya Ofisi na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mipango hiyo ikiwemo bajeti na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020;

iv. Imesimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Ofisi kwa upande wa Pemba ikiwemo Programu ya TASAF na Programu ya Kikabiliana na Maafa.

v. Imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za serikali Pemba ikiwemo ziara za Kamati za Baraza la Wawakilishi, Miradi inayotekelezwa kupitia fedha za kuchochea Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo (ZCDF) na mafunzo juu ya Sheria za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo;

vi. Imeratibu shughuli za kukabiliana na maafa Pemba ikiwemo kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya kijamii juu ya kujiandaa na kukabiliana na maafa, kaguzi katika maeneo mbalimbali, mikutano ya wadau na utoaji wa huduma na vifaa vya kibinaadamu katika maeneo yaliyopatwa na majanga;

vii. Imeratibu shughuli za Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizotekelezwa Pemba na kuwasafirisha wananchi 1,000 wa Mikoa miwili ya Pemba kushiriki maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi yaliyofanyika katika Uwanja wa Amaan, Unguja.

viii. Imeratibu shughuli za Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Kwanza wa Chama cha Afro Shirazi kwa kuendelea kutunza kaburi la aliyekuwa Waziri Kiongozi Mstaafu na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Dkt. Omar Ali Juma na kaburi la aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad. Aidha, Ofisi iliratibu dua na hitma zilizofanywa kwa Viongozi wetu hao walitangulia mbele ya haki;

93. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Ofisi Kuu Pemba iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 974,181,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2024 imetumia **Shilingi 572,268,552** ambazo ni sawa na **asilimia 77** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 59** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka. Aidha, kwa upande wa makusanyo ya mapato, Programu hii ndogo ilipangiwa kukusanya **Shilingi 22,542,495** kutokana na ukodishaji wa vifaa vya sherehe na hadi Machi, 2024 ilikusanya **Shilingi 6,660,000** ikiwa ni sawa na asilimia 37 kwa miezi tisa na **asilimia 30** kwa mwaka.

**C02 – BARAZA LA WAWAKILISHI**

94. **Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Afisi ya Baraza la Wawakilishi yanatekelezwa kupitia Programu Kuu mbili ambazo ni Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali na Programu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi.

**PROGRAMU KUU - (C0201): KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI**

95. **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu hii ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali inahusika na utekelezaji wa jukumu la msingi la Baraza la Wawakilishi ambalo ni kuhakikisha haki na utawala wa sheria vinatekelezwa Zanzibar ili kukuza demokrasia na uwakilishi wa wananchi. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2023/2024, Afisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeratibu Mkutano wa 12 ambao ulifanyika kuanzia tarehe 13 Septemba 2023, hadi tarehe 04 Oktoba 2023, Mkutano wa 13 uliofanyika kuanzia tarehe 29 Novemba, 2023 hadi tarehe 8 Disemba, 2023 na mkutano wa 14 ambao ulifanyika kuanzia tarehe 14 Febuari hadi tarehe 01 Machi 2024. Katika mikutano hiyo, shughuli mbali mbali zilifanyika **(Kiambatisho Nam. 5)** ikiwemo kuwasilishwa na kujadiliwa Ripoti za Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kujadiliwa na kupitishwa Miswada minane ya Sheria **(Kiambatisho Nam. 6),** Hoja binafsi mbili za Wajumbe ziliwasilishwa na kujadiliwa, Ripoti ya Wajumbe watano wa Baraza la Wawakilishi wanaoliwakilisha Baraza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ripoti ya Mwaka ya Mamlaka ya Dawa za Kulevya, Ripoti ya Mapedekezo ya Mwelekeo wa Mpango wa Taifa, Ripoti ya Jitihada za Utekelezaji wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kwa mwaka 2022, Ripoti ya saba ya Utekelezaji wa Tume ya Maadili ya mwaka 2022/2023. Kadhalika, jumla ya maswali 357 ya msingi na maswali 778 ya nyongeza

yaliulizwa na Wajumbe wa Baraza na kupatiwa majibu na Serikali;

ii. Imetoa Semina mbali mbali kwa Wajumbe na Watendaji wa Baraza katika kipindi 2023/2024 **(Kiambatisho Nam. 7);**

iii. Imeratibu shughuli za kawaida za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi za ufuatiliaji wa kazi za Wizara na Taasisi za Serikali zilifanyika ambapo Kamati nane (8) zilifanya kazi hiyo Unguja, Pemba na Tanzania Bara. Kazi za Kamati zilifanywa kwa mzunguko wa mwezi Agosti na Oktoba, 2023 pamoja na mwezi Januari 2024.

## GRAMU KUU - (C0202): UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI

**96. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo mbili ambazo ni Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi na Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba. Lengo la Programu Kuu hii ni kuweka mazingira ya kazi yatakayowezesha Baraza la Wawakilishi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024) cha mwaka wa fedha 2023/2024, Afisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeendelea na shughuli za kiutawala ikiwemo kukamilisha uwekaji wa lifti ya jengo la Afisi ya Baraza la Wawakilishi, uwekaji wa kamera za ulinzi (CCTV), ukarabati wa kibanda cha walinzi pamoja na matengenezo mengine madogo ya jengo. Aidha, Afisi imeendelea na ununuzi wa vitendea kazi pamoja na matengenezo ya vyombo vya usafiri. Kwa upande wa Afisi ya Pemba kumefanyika matengenezo ya jengo la mkahawa wa Afisi na ukarabati wa nyumba ya Mheshimiwa Spika iliyopo Wete Pemba;

ii. Imeendelea kuwajengea uwezo watendaji wake ambapo katika kipindi hicho jumla ya watumishi 18 wameendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi. Aidha wafanyakazi 11 walipatiwa mafunzo ya wiki moja ya "Advanced Microsoft Excel" katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na wafanyakazi wawili wanaendelea na mafunzo ya ukalimani katika Chuo hicho.

97. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Programu zake Kuu mbili kwa mwaka wa fedha 2023/2024 iliidhinishiwa kutumia **Shilingi 26,000,200,000** kwa matumizi ya kawaida na hadi kufikia Machi 2024, Afisi imetumia **Shilingi 16,559,932,713** sawa na **asilimia 85** kwa fedha iliyopangwa miezi tisa na asilimia 64 kwa mwaka.

## C03 – TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

98. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za chaguzi hapa Zanzibar. Jukumu hili linatekelezwa kupitia Programu Kuu mbili ambazo ni Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi na Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

### PROGRAMU KUU - (C0301): UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI

99. **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu hii inatekeleza jukumu la msingi la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo ni kuratibu na kusimamia chaguzi mbalimbali za nchi. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024) cha mwaka wa fedha 2023/2024, Tume ya Uchaguzi kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeandaa na kuendesha Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Mtambwe na Wadi ya Welezo uliofanyika tarehe 28 Oktoba 2023. Chaguzi hizo zilifanyika kufuatia vifo vya Mwakilishi (Mtambwe) na Diwani (Welezo) ambapo katika uchaguzi wa Jimbo la Mtambwe Mheshimiwa Mohamed Ali Suleiman alichaguliwa kuwa Mwakilishi na kwa uchaguzi wa Wadi ya Welezo Mheshimiwa Abdul-rahman Hassan Shaaban alichaguliwa kuwa Diwani kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2018. Matokeo ya chaguzi hizo yanaonekana katika Kiambatisho Nam. 8;

ii. Imeandaa Mpangokazi wa Uchaguzi Mkuu wa miaka mitatu (3) kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Aidha, imeandaa bajeti ya Uandikishaji Wapiga Kura wapya Awamu ya Kwanza na ya Pili pamoja na kuandaa bajeti ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 pamoja na mnyambuliko wa fedha "Cashflow" za Uchaguzi Mkuu 2025;

iii. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imefanya mapitio ya Kanuni za Uandikishaji na Uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura wapya za mwaka 2019, Maelekezo kwa Karani wa Uandikishaji Wapiga Kura wapya, Miongozo kwa Mawakala wa Vyama vya Siasa na Masheha;

iv. Imetoa Mafunzo ya awali ya Usimamizi na Uendeshaji Uchaguzi kwa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi na kufanya Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya Uandikishaji Wapiga Kura wapya Awamu ya kwanza 2023 na Uwekaji wazi Orodha wa Wapiga Kura;

v. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeimarisha mifumo ya uandikishaji kwa kuongeza utaratibu wa kusoma alama za vidole (Biometrics Fingerprints) za Wapiga Kura wakati wa uandikishaji ili kurahisisha zoezi hilo kufanyika kwa ufanisi na umakini zaidi;

vi. Imeendelea na kazi ya Uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kusahihisha taarifa za Wapiga Kura walioomba kusahihisha taarifa zao;

vii. Imefanya zoezi la Uandikishaji Wapiga Kura Wapya kwa Awamu ya Kwanza kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kwa Unguja na Pemba. Zoezi hilo lilianza tarehe 02 Disemba 2023 na kukamilika tarehe 15 Januari 2024 siku tatu kwa kila Wilaya;

viii. Iliendelea na kazi ya uwekaji wazi Orodha ya Wapiga Kura wapya walioandikishwa na Wapiga Kura walioomba kuhamishwa taarifa zao. Shughuli ya uwekaji wazi orodha ilifanyika tarehe 01- 07 Machi, 2024 kwa muda wa siku saba (7). Lengo la uwekaji wazi wa orodha hizo ni kuwapatia fursa Wapiga Kura kuweka pingamizi kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi namba 4 ya mwaka 2018. Jumla ya Wapiga Kura 345 Waliomba kuhamishiwa taarifa zao katika Wilaya zote za Unguja na Pemba na jumla ya vitambulisho 88 vimechapishwa kwa Wapiga Kura walioharibikiwa au kupoteza vitambulisho vyao. Takwimu za uandikishaji wa Wapiga Kura wapya Awamu ya Kwanza 2023 zinaonekana katika Kiambatisho Nam. 9;

ix. Imeendelea kusimamia na kuratibu utoaji wa Elimu ya Wapiga Kura katika shughuli mbali mbali za kiuchaguzi. Elimu hiyo ilitolewa hasa katika uendeshaji wa Uchaguzi mdogo wa Jimbo la Mtambwe, Uchaguzi Mdogo Wadi ya Welezo, zoezi la uandikishaji Wapiga Kura wapya, na uwekaji wazi orodha za Wapiga Kura wapya awamu ya kwanza na waliowasilisha maombi yao ya uhamisho. Elimu hiyo ilitolewa kwa kutoa taarifa kwa viongozi wa Wilaya, kutoa elimu katika Taasisi za Elimu na skuli mbali mbali za Serikali na Binafsi kwa Unguja na Pemba, kutoa elimu katika Shehia tofauti za Unguja na Pemba kupitia gari la matangazo (road show), na kuendesha vipindi vya Redio na Televisheni (TV). Aidha,

Elimu ilitolewa kupitia vipeperushi, mitandao ya kijamii na tovuti ya Tume pamoja na kuendesha mikutano ya wadau na matangazo mbali mbali;

x. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ikiwa ni mwanachama wa Jumuiya mbali mbali za kiuchaguzi za Afrika na Dunia kwa ujumla imepata mialiko kwa Wajumbe na Watendaji wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kushiriki mikutano inayohusu shughuli za Uchaguzi. Katika kipindi cha miezi tisa (9) (Julai 2023 – Machi 2024) Wajumbe na Watendaji walishiriki mikutano kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nam. 10.**

**PROGRAMU KUU - (CO302): USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA ZA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR**

**100. Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu inahusika na uwekaji wa mazingira mazuri kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kutekeleza majukumu yake. Katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024) cha mwaka wa fedha 2023/2024, Tume ya Uchaguzi kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeratibu upatikanaji wa hati miliki za majengo ya Afisi Kuu, Afisi ya Uchaguzi ya Wilaya za Magharibi A, Kaskazini B na Kati;

ii. Imeanza kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Jengo jipya la Afisi Kuu ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Mradi huu umepangwa kugharimu **Shilingi 11,321,009,509** ikiwa ni pamoja na kodi ya ongezeko la thamani. Hadi kufikia Machi 2024 Mkandarasi ameshapatiwa **Shilingi 1,698,151,423** ambayo sawa na **asilimia 15** ya fedha za mradi. Fedha zote za mradi huu zinatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

iii. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imewaendeleza kielimu watendaji wake kwa lengo la kuleta ufanisi katika kazi

iv. Imepokea gari kumi na mbili (12) kati ya gari 16 zilizoombwa na kukubalika Serikalini. Aidha, Afisi imenunua vifaa mbali mbali kwa ajili ya kuendesha shughuli za kiutendaji na kulipia huduma mbali mbali ili kutekeleza majukumu ya Afisi kwa ufanisi;

v. Imeendelea kutumia mifumo mbali mbali ya Serikali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku ili kurahisisha utekelezaji wa kazi zake na kuendana na kasi ya ukuaji wa Teknolojia iliyopo nchini. Miongoni mwa mifumo inayotumika katika Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ni "e-Office", "ZSSF", "ZSHIF", Zan ajira, "HRMIS", "Payroll system", Zan Malipo, BAMAS, na "e-procurement";

vi. Imefanya ukarabati mdogo katika Afisi ya Uchaguzi ya Wilaya Magharibi "A" ambao umehusisha urekebishaji wa sakafu ya Afisi hiyo;

vii. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imefanya zoezi la ufuatiliaji na Tathmini kwa shughuli mbali mbali zikiwemo:

   a. Tathmini ya Uchaguzi mdogo wa Jimbo la Mtambwe na Wadi ya Welezo,

   b. Tathmini ya ziara ya Wajumbe wa Tume katika Afisi za Tume ya Uchaguzi Zanzibar,

   c. Tathmini ya Mikutano ya Wadau Unguja na Pemba,

   d. Ufuatiliaji na Tathmini ya Uandikishaji Wapiga Kura Wapya

101. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kupitia Programu zake Kuu mbili kwa mwaka wa fedha 2023/2024 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 3,361,500,000** kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2024, Afisi imetumia jumla ya **Shilingi 2,568,658,778** sawa na **asilimia 91** kwa miezi tisa na **asilimia 76** kwa mwaka.

102. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilipangiwa kukusanya **Shilingi 10,000,000** na hadi kufika Machi 2024, fedha zilizokusanywa ni **Shilingi 4,657,000** sawa na **asilimia 66** ya fedha zilizotengwa kukusanya kwa miezi tisa na **asilimia 47** ya fedha zilizotengwa kukusanya kwa mwaka.

### UTEKELEZAJI KIFEDHA

103. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kupitia Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 75,316,157,000** ambapo **Shilingi 57,669,700,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 17,646,457,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2024, Ofisi imetumia **Shilingi 38,757,279,939** kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 88 kwa fedha zilizopangwa kutumika kwa miezi tisa na asilimia 67 fedha zilizopangwa kutumika kwa mwaka. Aidha, kwa upande wa kazi za maendeleo, Ofisi imepata **Shilingi 9,323,768,246** ikiwa ni **asilimia 70** ya kiasi kilichopangwa kwa miezi tisa na asilimia 53 kwa fedha zilizopangwa kwa mwaka. Kati ya fedha zilizopatikana **Shilingi 9,298,768,246** ni mchango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **Shilingi 25,000,000** ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar **(Kiambatisho Nam. 11 na Nam. 12).**

104. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Ofisi ilipangiwa kukusanya Shilingi 85,252,000 na hadi kufika Machi 2024, fedha zilizokusanywa ni Shilingi 33,722,600 sawa na asilimia 49 ya fedha zilizotengwa kukusanya kwa miezi tisa na asilimia 40 ya fedha zilizotengwa kukusanya kwa mwaka (Kiambatisho Namba 13).

**MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

105. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, pamoja na taasisi zake kwa mwaka 2024/2025 itaendelea kutekeleza na kusimamia Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14. Kupitia Programu hizo, Ofisi imepanga kutekeleza yafuatayo: -

## C01 – OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

**PROGRAMU KUU - (PC0101): URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

**Programu Ndogo (SC010101): Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais**

106. **Mheshimiwa Spika,** Program hii ina Progaramu Ndogo moja ya Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais yenye lengo la kuimarisha utendaji wa kazi kwa Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais. Matarajio ya muda mrefu ya program hii ni kuwepo huduma bora kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi kupitia Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais imepanga kufanya yafuatayo:-

i. Kuratibu ziara 60 za ndani na ziara 2 za nje ya Nchi za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya

kufuatilia na kuhamasisha shughuli za maenedeleo na kujenga uhusiano mwema wa kisiasa na kiuchumi;

ii. Kuimarisha ushirikiano na uhusiano mwema baina ya Zanzibar na nchi na mashirika ya ndani na Kimataifa kwa kuratibu mikutano baina ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Raisi na Mabalozi, Wawekezaji na Wageni Mashuhuri;

iii. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais zinazolenga kuleta maendeleo katika jamii;

iv. Kuyafanyia kazi malalamiko, migogoro na kero za wananchi kwa kushirikiana na Taasisi husika;

v. Kuratibu na kufuatilia matengenezo katika makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais yalioko Dar – Es - Salaam, Dodoma, Pemba na Mazizini Unguja;

vi. Kuratibu vikao vya uwasilishaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Wizara zote za SMZ vinavyofanyika kila baada ya miezi mitatu;

**107. Mheshimiwa Spika,** ili Programu hii ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais itekeleze kazi zake kwa mwaka 2024/2025, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 1,849,148,100** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,241,644,100** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na michango inayoambatana nayo na **Shilingi 607,504,000** ni kwa matumizi mengineyo.

**PROGRAMU KUU - (PCO102): URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI**

**108. Mheshimiwa Spika,** Programu hii lengo lake kubwa ni kuweka mfumo imara na endelevu wa uratibu wa shughuli

za Serikali, ambapo matarajio ya muda mrefu ni kupatikana kwa huduma bora za Serikali kwa jamii. Programu hii ina Programu Ndogo nne (4) ambazo ni Kuabiliana na Maafa, Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Uratibu wa Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Uratibu wa Shughuli za SMZ Dodoma.

**Programu Ndogo – SCO10201: Kukabiliana na Maafa**

**109. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa ina lengo la kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa kabla, wakati na baada ya kutokea. Kazi za Programu ndogo hii zinatekelezwa na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, kupitia fedha za kawaida kutoka kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kamisheni imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kufanya ukaguzi katika Taasisi za Serikali, binafsi na maeneo hatarishi yanayoweza kuathiriwa na maafa pamoja na kutoa elimu ya kujikinga, kujiandaa na kukabiliana na maafa;

ii. Kutoa elimu kwa makundi mbali ya jamii kuhusiana na masuala ya maafa;

iii. Kuandaa mikutano ya robo mwaka na wadau wote wanaoshughulikia masuala ya maafa ili kutathmini utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kukabiliana na maafa na kupanga mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza;

iv. Kuratibu na kutoa misaada ya kibinadamu katika matukio mbali mbali ya maafa yanayoweza kutokea;

v. Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa matukio ya maafa yanayotokea katika Wilaya za Unguja na Pemba;

vi. Kutoa tahadhari za mapema kwa wadau na jamii kwa jumla kupitia ujumbe wa pamoja (Bulk SMS) kupitia simu za mikononi;

vii. Kutoa mafunzo na miongozo mengine mbali mbali ya Kukabiliana na Maafa;

viii. Kuratibu shughuli za uendeshaji na utawala wa Taasisi.

**110. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kazi za kawaida kupitia fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo; Ofisi kupitia Programu Ndogo hii ya Kukabiliana na Maafa imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kujenga jengo la ghorofa mbili (2) Unguja na Pemba litakalojumuisha ghala, kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura na Ofisi za Kamisheni;

ii. Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Kukabiliana na Maafa wa Mwaka 2019-2024 na kupata Mpango mpya wa 2024-2029.

iii. Kuandaa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kukabiliana Maafa;

iv. Kuimarisha Mfumo wa taarifa za Kukabiliana na Maafa (Disaster Management Information System);

v. Kutoa elimu ya maafa kwa Taasisi za Serikali na binafsi na makundi ya jamii.

**111. Mheshimiwa Spika,** ili Programu ndogo ya Kukabiliana na Maafa itekeleze kazi zake kwa mwaka 2024/2025, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 1,865,600,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 942,200,000** kwa ajili ya malipo ya mishahara, **Shilingi 793,400,000** kwa matumizi mengineyo kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na

**Shilingi 130,000,000** kazi za matumizi mengineyo kupitia fedha za washirika wa maendeleo.

**Programu Ndogo – SCO10202: Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa**

**112. Mheshimiwa Spika,** Programu hii Ndogo ina jukumu la kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na shughuli za kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa. Kazi za Programu hii zinatekelezwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi kupitia Programu ndogo hii imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuratibu Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964;

ii. Kuendelea kulifanyia matengenezo jengo la Idara ili kuweza kupatikana kwa nafasi kwa ajili ya wafanyakazi na vifaa vya sherehe;

iii. Kuratibu Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Kwanza wa Chama cha Afro Shirazi na Siku ya Kumbukumbu ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume;

iv. Kuratibu ushiriki wa Wananchi na Viongozi katika Maadhimisho ya Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Sherehe za Uhuru wa Tanzania Bara pamoja na Siku ya Mashujaa;

v. Kununua vifaa vya sherehe ikiwemo, mashamiana, viti, meza na bendera kwa ajili ya Sherehe za Kitaifa;

vi. Kuimarisha huduma za usafiri kwa kununua gari kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

vii. Kusimamia shughuli za utendaji za Idara ikiwemo mafunzo kwa watumishi, ununuzi wa nyenzo na vifaa vya ofisi na ulipaji wa huduma zinazotolewa kwa Idara.

**113. Mheshimiwa Spika,** ili Programu ndogo ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa itekeleze kazi zake kwa mwaka 2024/2025, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 1,532,366,588** kwa matumizi ya kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **Shilingi 312,595,584** kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 1,219,771,004** kwa matumizi mengineyo.

**Programu Ndogo – SCO10203: Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

**114. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii ina jukumu la kuratibu shughuli za SMZ, mambo ya muungano, utafiti kitaifa pamoja na kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) hapa Zanzibar. Programu hii ndogo inayotekelezwa na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, katika mwaka wa fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuratibu Utekelezaji wa Shughuli za SMZ kwa kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 na Utekelezaji wa Maagizo na Ahadi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa; Shughuli za utoaji wa vibali vya Utafiti Zanzibar; Kusimamia Utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo;

ii. Kuanzisha Mfumo wa “Dash-board” wa Uratibu wa Shughuli za Serikali ambao utajumuisha uandaaji na uwasilishaji wa taarifa zinazohusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020, utekelezaji wa

maagizo na ahadi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa; utoaji wa vibali vya utafiti Zanzibar na utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo;

iii. Kuratibu Masuala ya Muungano kwa kuendelea kuratibu na kusimamia vikao vya Utatuzi wa Hoja za Muungano; kuratibu na kusimamia ushirikiano baina ya Wizara na Taasisi za SMZ na SJMT; kusimamia utekekelezaji wa Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar; na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano;

iv. Kuratibu masuala ya sera na siasa kwa kusimamia shughuli za kisiasa; kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera za Kisekta za SMZ na kuratibu Shughuli za Baraza la Wawakilishi.

**115. Mheshimiwa Spika,** Programu hii Ndogo vilevile itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini TASAF ukihusisha kipengele cha Uhaulishaji Fedha kwa Kaya Masikini; Mpango wa Kuweka Akiba na Kukuza Uchumi wa Kaya; Uratibu wa Ruzuku ya Uzalishaji; Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu; na Miradi ya Kutoa Ajira za Muda.

**116. Mheshimiwa Spika,** Programu hii pia itahusika na shughuli za kiutawala za Mpango wa TASAF kwa kuandaa vikao viwili vya Kamati ya Uongozi (Steering Committee) na vikao viwili vya Kamati Tendaji (Management Committee); Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa TASAF baina ya Zanzibar na Tanzania bara; Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya TASAF; na Kusimamia uendeshaji wa Shughuli za TASAF Unguja na Pemba.

**117. Mheshimiwa Spika,** ili Programu Ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itekeleze kazi zake kwa mwaka 2024/2025, naliomba Baraza lako Tukufu

liidhinishe jumla ya **Shilingi 32,400,697,490** ambapo **Shilingi 2,080,589,420** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 30,320,108,070** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo (Programu ya TASAF). Kati ya **Shilingi 2,080,589,420** za kazi za kawaida, **Shilingi 735,708,420** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 1,344,881,000** ni kwa matumizi mengineyo yanayohusisha pia **Shilingi 1,059,230,000** za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Aidha, kati ya **Shilingi 30,320,108,070** za kazi za maendeleo, **Shilingi 100,000,000** ni mchango wa SMZ na **Shilingi 30,220,108,070** ni mchango wa washirika wa Maendeleo.

**118.** Vilevile, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya **Shilingi 23,125,000,000** ikiwa ni ruzuku kwa ajili Idara ya Uhamiaji, Zanzibar.

**Programu Ndogo – SCO10204: Shughuli za SMZ Dodoma**

**119. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Shughuli za SMZ Dodoma ina lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa taasisi za SMZ kwa upande wa Tanzania Bara pamoja na kukuza na kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali/Taasisi za SMZ na SJMT, Washirika wa Maendeleo, Afisi za Kibalozi na asasi nyengine za kimataifa. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Programu hii Ndogo imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuratibu upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanapokuwa Tanzania Bara ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa urahisi na ufanisi ikiwemo usafiri;

ii. Kuratibu upatikanaji wa VISA kwa ajili ya Viongozi wa SMZ wanaotarajiwa kusafiri nje ya nchi;

iii. Kuratibu na kushiriki vikao vitano (5) baina ya Viongozi wa SMZ na Taasisi na Jumuiya za Kimataifa;

iv. Kuhamasisha taasisi za Serikali juu ya kutumia huduma zinazotolewa na Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma kwa kufanya warsha 1, kufanya kongamano la Maadhimisho ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Mwaka 1964, kuhudhuria katika Tamasha la Kimataifa la Biashara wakati wa Maadhimisho ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tamasha la Biashara la Saba Saba Dar es Salaam, kufanya vipindi viwili (2) vya Televisheni ya ZBC;

v. Kufanya utafiti wa kutathmini utaoji wa huduma za Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma;

vi. Kuratibu na kushiriki vikao 80 vya Ofisi na Wizara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**120.** **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar-Dodoma itekeleze kazi zake kwa mwaka 2024/2025, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 2,041,747,684.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 604,109,684** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 887,638,000** kwa matumizi mengineyo. Aidha, **Shilingi 550,000,000** ni kwa matumizi ya kazi za maendeleo ya mradi wa ukarabati mkubwa wa Ofisi ya Uratibu Dar es Salaam.

## PROGRAMU KUU - (PCO104): UENDESHAJI NA URATIBU WA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

**121.** **Mheshimiwa Spika,** lengo la Programu hii ni kuimarisha mazingira bora ya wafanyakazi, usimamizi wa mipango na shughuli za Ofisi ili kutoa huduma bora kwa jamii. Programu hii kuu ina Programu Ndogo tatu ambazo ni Uongozi na Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu na Utekelezaji wa Shughli za Ofisi, Pemba.

## Programu Ndogo – CO10401: Uongozi na Utawala

**122. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kusimamia na kuweka mazingira bora ya kazi na kutoa huduma bora za uendeshaji za kila siku pamoja na kusimamia rasilimali za Ofisi na maslahi ya wafanyakazi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Programu hii Ndogo pamoja na mambo mengine, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

Kusimamia maslahi na stahiki za wafanyakazi wa Ofisi kwa mujibu wa taratibu;

i. Kuratibu na kusimamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi katika kada na ngazi mbali mbali ndani na nje ya Nchi;

ii. Kuratibu na kusimamia upatikanaji wa vifaa na huduma za uendeshaji wa Ofisi;

iii. Kuratibu na kusimamia vikao vya utendaji kazi vya Ofisi vikiwemo vya Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji na Vikao vya Bodi ya Zabuni na Kamati ya Ukaguzi;

iv. Kuratibu na kusimamia huduma katika Ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul Wakil;

v. Kutoa mafunzo ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2014 kwa watumishi wa Ofisi;

vi. Kujenga na kuimarisha miundombinu ya uokozi wakati wa dharura katika jengo la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Vuga.

**123. Mheshimiwa Spika,** ili Programu ndogo ya Uongozi na Utawala itekeleze kazi zake kwa mwaka 2024/2025, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 1,854,385,802** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,118,473,802** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara, na S**hilingi 735,912,000** kwa matumizi mengineyo.

**Programu Ndogo – CO10402: Mipango, Sera na Utafiti**

**124. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti inahusika na kuandaa na kusimamia mipango na bajeti na pamoja na kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Ndogo hii imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti, mipango pamoja na miradi ya maendeleo ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

ii. Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Programu/miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Idara/Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na kazi za kawaida za Ofisi;

iii. Kuratibu uandaaji wa mapitio ya Sera, Sheria na Miongozo inayohusu shughuli zinazotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

iv. Kuratibu na kuandaa Vikao vya Mashirikiano baina ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar na Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

v. Kujenga uwezo kwa Maafisa Ufuatiliaji na Tathmini na Maafisa Mipango wa Idara/Taasisi za Ofisi ya Makamu

wa Pili wa Rais juu ya ufuatiliaji na tathimini wenye kutoa matokeo (Results Base Monitoring and Evaluation);

vi. Kuratibu na kusimamia tafiti zinazofanywa na Idara na Taasisi zilizomo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

vii. Kuratibu na kutoa mafunzo juu ya uandaaji na ufanyaji wa tafiti ndogo (Rapid Assesssment);

viii. Kuratibu na kuandaa Mpango Mkakati wa Takwimu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

ix. Kufanya mapitio ya nyenzo za kukusanyia taarifa za takwimu za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

x. Kusimamia shughuli za Kitengo cha Uratibu na Usimamizi wa Kitaifa wa Mfuko wa Fedha wa Dunia (ZGFCCM);

xi. Kuratibu utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Nyumba za Makamu wa Pili wa Rais Tibirinzi Pemba na Osterbay Dar es Salaam;

xii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mafunzo ya muda mfupi wa Idara.

**125. Mheshimiwa Spika,** ili Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti itekeleze kazi zake kwa mwaka 2024/2025, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 5,210,242,628** kwa matumizi ya kazi za kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 306,339,628** kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 199,903,000** kwa matumizi mengineyo. Aidha, **Shilingi 4,500,000,000** kwa mtumizi ya Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na **Shilingi 204,000,000** kwa ajili ya shughuli za Uratibu na Usimamizi wa Kitaifa wa Mfuko wa Fedha wa Dunia (ZGFCCM).

**Programu Ndogo – CO10403: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi – Pemba**

**126. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba inahusika na kuratibu shughuli za Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba na kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na usimamizi wa shughuli za Ofisi kwa jumla. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Programu hii Ndogo imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyiakazi na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba;

ii. Kuratibu ziara na shughuli za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Pemba;

iii. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi saba (7) na muda mfupi wafanyakazi wawili (2) wa Ofisi Pemba;

iv. Kuandaa mipango ya Ofisi na bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

v. Kuimarisha kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Program ya Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba;

vi. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali Pemba;

vii. Kuratibu shughuli za kukabiliana na maafa na kutoa elimu kwa jamii juu ya kujiandaa na kukabiliana na maafa Pemba;

viii. Kuratibu shughuli za sherehe na maadhimisho ya kitaifa na shughuli za kuwaenzi viongozi wakuu wa kitaifa Pemba;

127. **Mheshimiwa Spika** ili Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba itekeleze kazi zake kwa mwaka 2024/2025, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 953,319,782** kwa matumizi ya kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **Shilingi 690,528,782** kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 262,791,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

## C02 – BARAZA LA WAWAKILISHI

**PROGRAMU KUU - (*CO201*): KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI NA PROGRAMU KUU - (CO202): UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

128. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali ina jukumu la kuhakikisha haki na utawala wa sheria unatelekelezwa Zanzibar. Matarajio yake ya muda mrefu ni kukua kwa demokrasia na uwakilishi wa wananchi katika kusimamia na kufuatilia shughuli za Serikali. Huduma zinazotolewa ni kujadili, kurekebisha na kupitisha miswada ya Sheria, kusimamia utendaji wa taasisi za Serikali na kujadili na kupitisha bajeti ya Serikali.

129. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Programu Kuu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi ina jukumu la kuweka mazingira mazuri ya kazi, kuwajengea uwezo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wa Afisi ya Baraza ili kuongezeka kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Baraza na Afisi ya Baraza la Wawakilishi.

130. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, Programu hizi Kuu ambazo shughuli zake zinatekelezwa na Afisi ya Baraza la Wawakilishi zimepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuratibu Mikutano minne (4) ya kila mwaka ya Baraza la Wawakilishi;

ii. Kuratibu shughuli za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi;

iii. Kuendelea kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wa Afisi ya Baraza ili kukuza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao;

iv. Kutoa taaluma kwa umma kuhusu shughuli za Baraza kupitia vipindi vya Redio na Televisheni;

v. Kujenga mazingira mazuri kwa Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi ili iweze kusimamia majukumu yake yanayohusu Utumishi wa Baraza.

vi. Kuendelea kuimarisha mazingira ya Baraza kwa kufanya matengenezo ya kawaida ya majengo ya Afisi ya Baraza na nyumba za makaazi ya Mheshimiwa Spika.

vii. Kuanza utekelezaji wa mradi wa utanuzi wa jengo la Afisi ya Barara la Wawakilishi, Chukwani.

131. **Mheshimiwa Spika,** ili Afisi ya Baraza la Wawakilishi iweze kutekeleza malengo yake hayo kwa ufanisi zaidi, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe **Shilingi 30,873,400,000** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 9,327,710,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 21,545,690,000** ni kwa kazi nyenginezo.

## C03 – TUME YA UCHAGUZI

**132.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka wa Fedha 2024/2025 Tume ya Uchaguzi itaendelea kutekeleza Programu zake Kuu mbili ambazo ni Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi na Programu ya Usimamizi wa Kazi za Utawala za Uendeshaji wa shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

**PROGRAMU KUU - (C0301): UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI**

**133.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi inahusika kupanga na kutekeleza jukumu la msingi msingi la Tume ya Uchaguzi la kuratibu na kuenesha chaguzi hapa nchini. Kwa mwaka fedha 2024/2025, Tume ya Uchaguzi kupitia Programu hii imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuandikisha Wapiga Kura Wapya katika Daftari la Kudumu kwa awamu ya pili;

ii. Kuendelea kutoa elimu ya Wapiga Kura kwa makundi mbali mbali ya jamii;

iii. Kufanya mapitio ya miongozo mbali mbali inayohusiana na shughuli za uchaguzi;

iv. Kuendelea na matayarisho ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

**PROGRAMU KUU - (CO302): USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA ZA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR**

**134.** **Mheshimiwa Spika,** Katika Programu ya Usimamizi wa Shughuli za Utawala za Afisi ya Tume ya Uchaguzi, Tume

ya Uchaguzi mwaka ujao wa fedha wa 2024/2025 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuendelea na uratibu na usimamizi wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la kisasa la Afisi Kuu ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Maisara;

ii. Kujenga majengo mapya ya Afisi za Wilaya za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar;

iii. Kununua vifaa na huduma mbali mbali kwa ajili ya kuwezesha utendaji na kuleta ufanisi katika Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar;

iv. Kuendelea kusomesha na kuwaendeleza kitaaluma wafanyakazi wa Tume katika kada na ngazi mbali mbali;

v. Kuimarisha majengo ya Afisi za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

**135. Mheshimiwa Spika,** ili Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iweze kutekeleza malengo ya Programu zake naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 5,380,000,000** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 4,800,400,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 580,400,000** ni kwa kazi nyenginezo.

**UKUSANYAJI MAPATO**

**136. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imepangiwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 67,180,000** kupitia Mafungu ya C01 (Ofisi Makamu wa Pili wa Rais -Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa na Afisi Kuu Pemba) na C03 (Tume ya Uchaguzi) kwa mchanganuo ufuatao:-

| | |
|---|---|
| Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 32,710,000 |
| Afisi Kuu Pemba | 19,590,000 |
| Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | 14,879,000 |
| **Jumla** | **67,179,000** |

## HITIMISHO

**137. Mheshimiwa Spika,** naomba kumalizia hotuba hii, kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa muda wa kutosha kuwasilisha mapendekezo yetu ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025; lakini pili kwa upekee naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mheshimiwa Machano Othman Said, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mfenesini kwa ushauri na maelekezo yao kwetu ambayo kwa hakika yametusaidia katika kutekeleza kazi zetu kwa ufanisi na mafanikio makubwa. Tunaishukuru zaidi kwa kuipokea, kuipitia na hatimae kuridhia hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuwasilishwa katika Baraza hili.

**138. Mheshimiwa Spika,** Nchi yetu imeendelea kujenga na kudumisha ushirikiano mkubwa na mashirika, jumuiya na taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa. Aidha nchi mbalimbali tumekuwa tukishirikiana nazo katika harakati zetu za kimaendeleo katika nyanja zote. Naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana washirika wetu hawa wa maendeleo kwa misaada yao ya kifedha na kitaalamu au kiufundi ambayo imetusaidia katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Miongoni mwa mashirika hayo ya kimataifa ni Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Benki ya Dunia, Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo UNDP, UNICEF, UNFPA, WHO, WFP, UN-Women, FAO na UNAIDS. Mashirika mengine ni Benki ya Maendeleo ya Afrika, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu Malaria na UKIMWI, BADEA, GPE, KOICA, Sida- Sweden. Aidha tunazishukuru nchi za China, Cuba, India, Japan, Marekani, Oman, Umoja wa Falme za Nchi za Kiarabu (UAE),

na wengine wote ambao tumeshirikiana nao katika miradi ya maendeleo kwa manufaa ya nchi yetu na wananchi wake.

**139. Mheshimiwa Spika,** tunaahidi kuendelea na wenzetu hawa na wengine watakaojitokeza ili kwa pamoja tuimarishe huduma za kiuchumi na kijamii katika nchi yetu.

**140. Mheshimiwa Spika,** Vilevile, tunatoa shukurani zetu nyingi kwa wafanyabiashara na taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa kuendelea kusaidiana na Serikali katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. Serikali itaendelea kuhakikisha kunakuwepo na mazingira mazuri na wezeshi ya kutekeleza kazi zao hapa nchini.

**141. Mheshimiwa Spika,** Ofisi yetu imekuwa ikifanyakazi kwa karibu na kwa mashirikiano makubwa wenzetu Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa dhati kabisa naomba nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wa Ofisi na Wizara hizi kwa mashirikiano makubwa wanayotupa katika kutekeleza majukumu yetu.

**142. Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru sana Viongozi wenzangu na watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Namshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi) Mheshimiwa Hamza Hassan Juma kwa kunisaidia kuisimamia Ofisi yetu. Aidha, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Islam Seif Salum na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Salhina Mwita Ameir ambao kwa kushirikiana na Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zilizomo katika Ofisi yetu wamekuwa wakitekeleza kazi za Ofisi yetu kwa uweledi na umahiri mkubwa na hatimae kufanikiwa kufikia malengo yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwangozea uwezo na maarifa zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao.

**143. Mheshimiwa Spika,** mwisho, lakini si kwa umuhimu naomba niwapongeze na kuwashukuru sana wenzetu wanahabari kwa kuendelea kuwapa taarifa wananchi juu ya masuala mbalimbali yanayotokea hapa nchini zikiwemo shughuli mbalimbali za Serikali ikiwa ni pamoja na Mikutano yetu hii ya Baraza la Wawakilishi. Wenzetu hawa wamekuwa ni kiungo baina ya Serikali na wananchi waliopo nchini na wale waliopo nje. Kwa upande wetu Serikali tutaendelea kushirikiana nao ili wananchi na wadau wengine wapate habari za uhakika. Nawaomba sana waendelee kutumia taaluma yao kuifanya kazi yao kwa weledi zaidi katika kuwahabarisha, kuwaelimisha na kuwaburudisha wananchi.

**144. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 107,086,308,074** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14 nilizozielezea hapo awali. Mchanganuo wa fedha hizo kwa Programu ni kama zinavyoonekana katika **Kiambatisho Nam. 14** na kwa mafungu ni kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais | **Shilingi** | **70,832,508,074** |
| 2. Afisi ya Baraza la Wawakilishi | **Shilingi** | **30,873,400,000** |
| 3. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | **Shilingi** | **5,380,400,000** |
| **JUMLA KUU** | **Shilingi** | **107,086,308,074** |

**145. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**MHESHIMIWA HEMED SULEIMAN ABDULLA**
**MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR**

*Kiambatisho Nam. 1*.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UJENZI (TARGETED INFRASTRUCTURES) KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2024**

| NA. | SHEHIA | JINA LA MRADI | FEDHA YOTE YA MRADI ILIYOPATIKANA | FEDHA ILIYOTUMIKA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kizimkazi Mkunguni | Ukarabati wa Majengo ya Skuli ya Kizimkazi Mkunguni. | 277,232,142.86 | 56,119,142.86 | Mradi umekamilika kwa asilimia 99. |
| 2. | Donge pwani | Ujenzi wa Jengo la Wazazi (Maternity ward). | 158,927,708.88 | 9,658,600.00 | Mradi umekamilika kwa asilimia 99. |
| 3. | Uzi | Ujenzi wa Kituo cha Afya Daraja la Pili | 288,416,626.78 | 33,500,000.00 | Mradi unaendelea na utekelezaji na umefikia asilimia 88. Ofisi imewasilisha maombi ya fedha ya ziada za ukamilishaji wa ujenzi. |
| 4. | Bambi | Ujenzi wa Ukumbi wa Mitihani Skuli ya Bambi. | 60,267,857.14 | 34,569,500.00 | Mradi unaendelea na utekelezaji na umefikia asilimia 42. Ofisi imewasilisha maombi ya awamu ya pili ya fedha za ujenzi. |
| 5. | Upenja | Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Upenja | 143,817,473.21 | 1,396,000.00 | Mradi umeanza kutekelezwa tarehe 18, Septemba 2023 na umefikia asilimia 12 ya utekelezaji. |
| | | | **928,661,808.87** | **135,243,242.86** | |

*Kiambatisho Nam. 2.*

**IDADI YA VIKUNDI VYA KUWEKA NA KUKUZA UCHUMI WA KAYA VILIVYOSAJILIWA KWA KIPINDI CHA JULAI HADI MACHI, 2024**

| NA | WILAYA | IDADI YA VIKUNDI |
|---|---|---|
| 1. | Kusini Unguja | 59 |
| 2. | Kati | 101 |
| 3. | Magharibi A | 58 |
| 4. | Magharibi B | 49 |
| 5. | Mjini | 25 |
| 6. | Kaskazini A | 50 |
| 7. | Kaskazini B | 47 |
| **JUMLA KUU** | | **389** |

*Kiambatisho Nam. 3*.

**VIKAO VYA MASHIRIKIANO YA KAZI BAINA YA WIZARA ZA SMZ, SMT, OFISI ZA KIBALOZI, TAASISI NA JUMUIYA ZA KIMATAIFA**

| Nam | Tarehe | Kikao | Lengo |
|---|---|---|---|
| 1. | 17//07/2023 | Kikao cha Utekelezaji yatokanayo na ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Katalon Novak Rais wa Hungary. | Ufuatiliaji wa utekelezaji wa yatokanayo na ziara ya Mheshimiwa Rais wa Hungary. Kiliandaliwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kikao kilifanyika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) |
| 2. | | Kikao cha kwanza cha maandalizi ya maadhimisho ya miaka 60 ya uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na China. Maadhimisho ambayo yatafanyika kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024. | Ajenda kuu ya kikao hicho ilikuwa ni kujadili utekelezaji wa maadhimisho ya miaka 60 ya uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na China. |
| 3. | 23/08/2023 | Kikao kati ya Halmashauri ya Wilaya Kongwa na Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za Serikali Dodoma. | Kupanga na namna Wilaya ya Kongwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitakavyoshirikiana katika nyanja mbalimbali za maendeleo |
| 4. | 31/08/2023 | Kikao cha GPS baina ya Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Afisi ya Rais – Fedha na Mipango ya Zanzibar | Kujadiliana kwa pamoja juu ya suala la GPS kutoka 4.5% hadi 9%. |
| 5. | 01/09/2023 | Kikao cha ngazi ya wataalam kuhusu Mpango kazi wa mchakato wa utungwaji na marekebisho ya sheria za uchaguzi na vyama vya siasa. | Majadiliano juu vifungu vya sheria husika |
| 6. | 04/09/2023 | Kikao ngazi ya Makatibu Wakuu cha kujadili Mpango kazi wa mchakato wa utungaji na marekebisho ya sheria za uchaguzi na vyama vya siasa. | Kujadili mapendekezo ya wataalamu juu vifungu vya sheria husika |
| 7. | | Kikao na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. | Kujadili changamoto ya viinua mgongo na pencheni ya watendaji ambao wamepoteza maisha wakiwa katika dhamana ya kulitumikia jeshi hilo. Aidha, kikao kilijadili suala la ajira na upandishaji vyeo kwa vijana kutoka Zanzibar. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8. | 25/08/2023 | Kikao cha Wadau juu ya yatokanayo na ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jijini ST. Petersburg, Urusi kuanzia tarehe 27 hadi 30 Julai 2023. | Kupitia na kujadili maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ziara aliyoifanya Nchini Urusi. Kikao kilifanyika Jijini Dodoma katika Ukumbi wa Mikutano Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliopo katika jengo la PSSSF. |
| 9. | 21-25/8/ 2023 | Ziara ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika Ofisi Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma, TASAF na TAKUKURU. | Kujifunza namna Ofisi hizo zinavyofanya kazi. |
| 10. | 17/8/2023 | Kikao cha kwanza cha dharura cha Kamati ya Kitaalamu ya Kudhibiti Madeni (TDMC). | Kupitia maombi ya mikopo na misaada inayotaka kuombwa na Serikali au Taasisi binafsi kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Kikao kilifanyika Dodoma Wizara ya Fedha na Mipango. |
| 11. | 04/8/2023 | Kikao cha Kamati ya kudumu ya mafunzo ya Shahada ya Uzamili na Programu ya Elimu ya Biashara kwa Vijana wa Afrika | Kumalizia hatua za mwisho za awamu ya kumi ambapo hatua iliyofikia ni kutoa taarifa za wanafunzi waliopata nafasi katika Programu ya Masomo ya Shahada ya Uzamili na mpango wa mafunzo ya vitendo (internship) unaoitwa “African Business Education for Youth (ABE Initiative)”. Kikao kilifanyika katika Ukumbi wa Hoteli ya Onomo, Jijini Dar es Salaam. |
| 12. | 15/11/2023 | Ziara ya Kamati ya Bajeti ya BLW kutembelea katika Taasisi zilizopo Tanzania bara ikiwemo; - Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Mamlaka ya Kusimamia Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA). | Kujifunza kwa kuona na kusikiliza juu ya utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13. | 15/12/2023 | Kikao cha tatu cha wataalam kwa ajili ya Maandalizi ya mkutano wa kwanza wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano (JPC) kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Angola. | Kujadili maandalizi ya ushiriki wan chi katika mkutano huo |
| 14. | 2-3/11/ 2023 | Kikao cha Pili cha Kamati ya Kitaalamu ya Kudhibiti Madeni (TDMC) kwa mwaka wa Fedha 2023/24 kilichofanyika katika Ukumbi wa Hazina Dodoma. | Kupitia na kujadili maombi ya mikopo. Kikao kilifanyika Dodoma Wizara ya Fedha na Mipango |
| 15. | 14/11/2023 | Kikao cha Pili cha Dharura cha TDMC 2023/24. | Kupitia na kujadili maombi ya mikopo. Kikao kilifanyika Dodoma Wizara ya Fedha na Mipango. |
| 16. | 11/12/2023 | Kikao cha Tatu cha Kawaida cha TDMC kwa mwaka 2023/2024 | Kupitia na kujadili maombi ya mikopo. Kikao kilifanyika Dodoma Wizara ya Fedha na Mipango. |
| 17. | 20 - 23/11/2023 | Ziara ya Kamati ya Ardhi, Mawasiliano na Nishati ya Baraza la Wawakilishi iliyotembelea Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Taasisi Teknolojia ya Ujenzi (ICoT) | Kujifunza nakubadilishana uzoefu wa shughuli mbali mbali zinazotekelezwa na Taasisi hizo. |
| 18. | 20-23/02/2024 | Ripoti ya ziara ya Afisa kiungo katika Wizara za SMZ zikiwemo Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Wizara ya Maji, Nishati na Madini na Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.. | Kuitangaza Ofisi pamoja na kumtambulisha Afisa Kiungo katika Wizara hizo. |
| 19. | 4-6/02/2024 | Ripoti ya ziara ya Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi Dodoma. Ziara hiyo ilifanyika Dodoma katika Tume ya Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto. | Kujifunza na kupata uzoefu kuhusu kuandaa Miundo ya Kiutumishi na Kitaasisi. |
| 20. | 07-21/01/2024 | Ripori ya Maadhimisho ya 10 ya Biashara katika wiki ya kuadhimisha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yaliyofanyika viwanja vya Nyamanzi, Wilaya ya Magharibi “B”, Zanzibar. | Kujadili ripoti |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 21. | 25/01 - 2/02/2024 | Ripoti ya kikao cha nne na cha tano vya Kamati ya Kitaalamu ya Kudhibiti Madeni (TDMC) kwa mwaka wa 2023/2024 | Kujadili miradi mbali mbali, miswaada na dhamana inayoombwa na Taasisi mbali mbali na kuikubali au kuikataa kulingana athari yake kwenye Uchumi wa Tanzania. Kikao hicho kilifanyika katika Ukumbi wa Hazina Dodom. |
| 22. | 14/01/2024 | Kikao cha Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Wanachi Tanzania. | Kujadili utoro wa waajiriwa wa Jeshi hilo wanaotokea Zanzibar ambao wengi wao wanatoroka baada ya kumaliza Mafunzo. Kikao hicho kilifanyika Makao Makuu ya Jeshi, Ngome Dar es Salaam. |
| 23. | 18/01/2024 | Kikao cha Wizara ya Mambo ya ndani na Jeshi la Uhamiaji. | Kusisitiza uwiano wa ajira kwa wananchi wa Zanibar wakati wakutangaza Ajira mpya. Kikao kilifanyika katika Wizara ya Mambo ya Ndani Mtumba. |
| 24. | 28/01/2024 | Kikao cha Wizara ya Fedha na Mipango (SMT) | Kujadili miradi inayohusisha upande mmoja ambayo Zanzibar huwa inakosa fursa. Kikao kilikubaliana kuwa kabla kupelekwa miradi kuwe na kikao cha pamoja. Kikao hicho kilifanyika Mtumba Dodoma. |
| 25. | 07/02/2024 | Kikao cha Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) | Kujadili sherehe za Muungano ikiwemo sehemu zitakapofanyika sherehe, vitu gani vya muhimu, mgeni Rasmi, Kauli mbiu, pia kikao kilikubaliana kuwa sherehe zifanyike kila mkoa. Kikao hicho kilifanyika Mtumba jijini Dodoma. |
| 26. | 10-16/03/2024 | Kikao cha Ofisi ya Waziri Mkuu | Kujadili miongozo ya Sherehe za Kitaifa ambapo kikao kilikubaliana kwamba sherehe zote zitakazofanyika Mwenyekiti akitoka Tanzania Bara Makamo Mwenyekiti atoke Zanzibar. Kikao kilifanyika Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 27. | 27-28/02/2024 | Kikao cha Wizara ya Elimu (SMT) | Kujadili Maadhimisho ya Sokoine ambapo mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kikao hicho kilifanyika Dodoma. |
| 28. | 29/12/2023 - | Kikao kazi cha Uandaji wa Kitabu cha Miaka sitini (60) ya Ofisi ya Makamu wa Rais toka kuanzishwa kwake ikiwa ni sehemu ya matunda ya Muungano wa Tanzania. | Kushiriki katika kutoa taarifa juu ya masuala ya muungano ndani kitabu hicho |

***Kiambatisho Nam. 4.***

**IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOPATIWA MAFUNZO YA MUDA MREFU**

| JINA LA IDARA/TAASISI | CHETI (CERTIFICATE) | | STASHAHADA (DIPLOMA) | | SHAHADA YA KWANZA (DEGREE) | | STASHAHADA YA UZAMILI (PGD) | | SHAHADA YA PILI (MASTERS) | | SHAHADA YA UZAMIVU (PHD) | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | M | F | M | F | M | F | M | F | M | F | M | F | |
| Afisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais | - | - | - | 1 | 2 | 2 | - | - | - | - | - | - | 5 |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | - | 1 | - | 1 | 1 | 5 | - | - | 1 | 1 | - | - | 10 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - | - | - | 1 | 2 |
| Idara ya Uratibu na Shughuli za Serikali | - | - | - | - | - | - | - | - | 2 | 3 | - | 1 | 6 |
| Afisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dodoma | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - | - | - | - | 1 |
| Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | - | - | 1 | - | - | 1 | - | - | - | 2 | - | - | 4 |
| Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | - | - | - | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - | 1 |
| Afisi Kuu - Pemba | - | - | 1 | 3 | 1 | 2 | - | - | - | - | - | - | 7 |
| **JUMLA KUU** | **-** | **1** | **2** | **5** | **4** | **12** | **-** | **-** | **4** | **6** | **-** | **2** | **36** |

*Kiambatisho Nam. 5.*

**SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA MIKUTANO MITATU KWA VIPINDI TOFAUTI KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA KIPINDI JULAI – MACHI, 2024**

| Nam. | Aina ya Hoja | Mtoa hoja |
|---|---|---|
| 1. | Ripoti ya Saba ya Utekelezaji wa Tume ya Maadili kwa mwaka 2022/2023 | Serikali |
| 2. | Hoja Binafsi ya Mjumbe Kuhusu Kuunga Mkono Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025 Katika Kipindi cha Miaka Mitatu ya Awamu ya Nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | Mh.Asha Abdalla Mussa |
| 3 | Ripoti za Kamati za Kudumu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 | Wenyeviti wa Kamati za Kudumu. |
| 4 | Ripoti ya mapendekezo ya mwelekeo wa mpango wa Taifa | Serikali |
| 5 | Ripoti ya Wajumbe watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Wajumbe 5 wanaoliwakilisha Baraza Bungeni |
| 6 | Ripoti ya Mwaka ya Mamlaka ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2022/2023. | Serikali |
| 7 | Ripoti ya Jitihada za utekelezajiwa wa kuzuia rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kwa mwaka 2022 | Serikali |

***Kiambatisho Nam. 6.***

**MISWADA ILIYOJADILIWA NA KUPITISHWA NA BARAZA LA WAWAKILISHI**

| Nam | Mswada |
|---|---|
| 1. | Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam.11 ya 2003 na Kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. |
| 2. | Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam.9 ya 2017 na Kutunga Sheria ya Mahakama za Kadhi na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. |
| 3. | Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Utoaji Leseni, Kudhibiti na Kusimamia Biashara ya Huduma Ndogo Ndogo za Fedha kwa ajili ya Kudumisha Utulivu, Usalama na Ubora wa Huduma Ndogo Ndogo za Fedha na Mambo Mengine Yansyohusiana na Hayo. |
| 4. | Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Nam.14 ya 2018 na Kutunga Sheria ya Uwekezaji Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo. |
| 5. | Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar na Kuweka mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. |
| 6. | Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar Kwa ajili ya Ununuzi, Utengenezaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. |
| 7 | Mswada wa Sheria ya kurekebisha Sheria mbali mbali na kuweka masharti bora ndani yake. |
| 8 | Mswada wa Sheria ya kuanzishwa Mamlaka ya Mawasiliano |
| 9 | Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu<br>Zanzibar Nam. 3 ya 2011 na kutunga Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kwa ajili ya kutoa Msaada wa Kifedha wa wanafunzi na mambo mengine yanayohusiana na hayo. |

*Kiambatisho Nam. 7.*

**SEMINA ZILIZOTOLEWA KWA WAJUMBE NA WATENDAJI WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

| NAM | SEMINA |
|---|---|
| 1 | Utaratibu wa kupitisha Miswada Maalum ya Sheria katika Kamati na Baraza |
| 2 | Matumizi ya Sheria ya Tafsiri Nam. 7 ya 1984 katika kuwasaidia Wajumbe kutekeleza majukumu yao ya kutunga Sheria. |
| 3 | Uchambuzi na Uchangiaji Huru wa Miswada inayotungwa Sheria Mpya ndani ya Baraza la Wawakilishi |
| 4 | Namna ya Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza wanavyotakiwa kuifanyia kazi Miswada ya Sheria katika Kamati zao |
| 5 | Maadili ya viongozi kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza majukumu yao. |
| 6 | Mafunzo kuhusu Sheria ya Manunuzi na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma. |
| 7. | Mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu huduma za fedha na Huduma zinazotolewa na Benki ya CRDB. |

*Kiambatisho Nam. 8.*

**MATOKEO YA UCHAGUZI MDOGO JIMBO LA MTAMBWE**

**NA WADI WELEZO**

| **JIMBO LA MTAMBWE** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **NA** | **JINA KAMILI** | **CHAMA** | **KURA HALALI ZA MGOMBEA** | **JUMLA YA KURA HALALI** | **KURA ZILIZOHARIBIKA** | **ASILIMIA YA K/HALALI** |
| **1** | MOHAMED ALI SULEIMAN | ACT | 2449 | 4045 | 155 | 60.54 |
| **2** | MOHAMED MASOUD RASHID | CHAUMA | 22 | | | 0.54 |
| **3** | HAMAD KHAMIS HAMAD | CCM | 1531 | | | 377.84 |
| **4** | SAID NASSOR HEMED | CUF | 43 | | | 1.06 |
| **WADI YA WELEZO** | | | | | | |
| **NA** | **JINA KAMILI** | **CHAMA** | **KURA HALALI ZA MGOMBEA** | **JUMLA YA KURA HALALI** | **KURA ZILIZOHARIBIKA** | **ASILIMIA YA K/HALALI** |
| **1** | OMAR SHAABAN DAFA | D-MAKINI | 136 | 3143 | 42 | 4.3 |
| **2** | ABDUL-RAHMAN HASSAN SHAABAN | CCM | 2841 | | | 90.4 |
| **3** | MOHAMED RAMADHAN VUAI | UPDP | 166 | | | 5.3 |

*Kiambatisho Nam. 9*

**TAKWIMU ZA WAPIGA KURA WALIOANDIKISHWA KATIKA AWAMU YA KWANZA UANDIKISHAJI 2023**

| Wilaya | | Idadi ya walioandikishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake | Wanaume | Jumla |
| 1. | Micheweni | 1,397 | 1,231 | 2,628 |
| 2. | Wete | 1,786 | 1,475 | 3,261 |
| 3. | Chake Chake | 2,021 | 1,695 | 3,716 |
| 4. | Mkoani | 1,309 | 1,253 | 2,562 |
| 5 | Kaskazini "A" | 4,044 | 3,221 | 7,265 |
| 6 | Kaskazini "B" | 2,125 | 1,836 | 3,961 |
| 7 | Magharibi "A" | 3,900 | 3,257 | 7,157 |
| 8 | Magharibi "B" | 4,973 | 4,078 | 9,051 |
| 9 | Kati | 2,488 | 2,197 | 4,685 |
| 10 | Kusini | 1,552 | 1,323 | 2,875 |
| 11 | Mjini | 5,845 | 4,877 | 10,722 |
| **Jumla** | | **31,440** | **26,443** | **57,883** |

*Kiambatisho Nam. 10*

**MIKUTANO YA KIUCHAGUZI WALIOHUDHURIA WAJUMBE NA WATENDAJI WA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR**

| NO. | AINA YA MKUTANO | ALIYEHUDHURIA | PAHALA |
|---|---|---|---|
| 1. | Uangalizi wa Uchaguzi Mkuu wa Zimbabwe | Mkurugenzi wa Uchaguzi na Mkuu wa Kurugenzi ya Utumishi, Mipango, na Utawala | Zimbabwe |
| 2. | Mkutano wa Kuidhinisha (Validation) Misingi na Mwongozo wa matumizi ya Dijitali na Mitandao ya kijamii katika Uchaguzi | Mkurugenzi wa Uchaguzi | Benin |
| 3. | Mkutano wa mwaka wa Umoja wa Tume za Uchaguzi za Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (ECF-SADC) na Maadhimisho miaka 25 ya Umoja huo | Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na Mkuu wa Kurugenzi ya Huduma za Uchaguzi | Afrika Kusini |
| 4. | Mkutano wa wadau wa Vyama vya Siasa | Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi na Mkurugenzi wa Uchaguzi | Dar-es-Salaam |
| 5. | Uzinduzi wa Misingi na Mwongozo wa matumizi ya Dijitali na Mitandao ya kijamii katika Uchaguzi | Mwenyekiti Wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Mkuu wa Kurugenzi ya Mipango, Utumishi na Utawala, pamoja Mkuu wa Kurugenzi ya Elimu ya Wapiga Kura na Mawasiliano kwa Umma. | Afrika kusini |
| 6. | Mjadala wa Miswada ya Sheria za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2023 | Mkurugenzi wa Uchaguzi na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. | Dodoma |
| 7. | Mafunzo kwa Watendaji wa Uchaguzi Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) katika Uchaguzi Mdogo wa Kata 22 za Tanzania Bara | Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Makamo Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Mkurugenzi wa Uchaguzi Mkuu wa Kurugenzi ya Mipango, Utumishi na Utawala, Mratibu wa Afisi ya Tume Pemba na Mkuu wa Kurugenzi ya Huduma za Uchaguzi | Morogoro na Tabora |

# TAARIFA YA UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA, OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS, KWA KIPINDI CHA JULAI, 23 HADI MACHI 20/24

| S/N | JINA LA PROGRAMU | JINA LA PROGRAMU NDOGO | IDARA/TAASISI HUSIKA | MAKISO KWA MWAKA | MAKISIO KWA MIEZI TISA | | | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA MIEZI TISA | | | ASILIMIA (%) KWA MIEZI TISA | ASILIMIA (%) KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | MISHAHARA | OC | JUMLA | MISHAHARA | OC | JUMLA | | |
| 1 | 1.Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais | 1.Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais | Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais | 1,631,251,000 | 833,347,500 | 420,721,000 | **1,254,068,500** | 871,202,353 | 169,254,000 | **1,040,456,353** | **83** | **64** |
| 2 | Uratibu wa Shughuli za Serikali | 2. Kukabiliana na Maafa | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | 1,581,510,000 | 631,350,000 | 573,880,000 | **1,205,230,000** | 680,864,415 | 302,489,900 | **983,354,315** | **82** | **62** |
| | | 3. Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa | Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 1,683,357,000 | 235,443,000 | 1,340,913,000 | **1,576,356,000** | 230,807,534 | 2,021,315,710 | **2,252,123,244** | **143** | **134** |
| | | 4. Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ | 925,969,000 | 491,784,750 | 199,483,250 | **691,268,000** | 528,129,860 | 116,807,000 | **644,936,860** | **93** | **70** |
| | | | Ruzuku kwa ajili ya Shughuli za Idara ya Uhamiaji | 18,499,900,000 | | 13,874,925,000 | **13,874,925,000** | | 12,333,264,333 | **12,333,264,333** | **89** | **67** |
| | | 5. Shughuli za SMZ Dar es Salaam | Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ, Dar es Salaam | 976,659,000 | 340,833,750 | 409,312,250 | **750,146,000** | 379,280,458 | 132,343,000 | **511,623,458** | **68** | **52** |
| 3 | Uendeshaji na Uratibu | 6. Uongozi na Utawala | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 1,592,483,000 | 748,824,750 | 452,727,501 | **1,201,552,251** | 742,078,839 | 292,101,619 | **1,034,180,458** | **86** | **65** |
| | | 7. Mipango, Sera na Utafiti | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 442,690,000 | 192,377,250 | 154,361,501 | **346,738,751** | 209,294,875 | 47,186,000 | **256,480,875** | **74** | **58** |
| | | 8. Ofisi Kuu Pemba | Ofisi Kuu Pemba | 974,181,000 | 570,489,000 | 171,947,010 | **742,436,010** | 500,268,552 | 72,000,000 | **572,268,552** | **77** | **59** |
| **Jumla ndogo** | | | | **28,308,000,000** | **4,044,450,000** | **17,598,270,512** | **21,642,720,512** | **4,141,926,886** | **15,486,761,562** | **19,628,688,448** | **91** | **69** |

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4 | Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali | 9. Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali | Baraza la Wawakilishi | 26,000,200,000 | 7,712,437,000 | 11,879,226,000 | **19,591,663,000** | 6,580,252,537 | 9,979,680,176 | **16,559,932,713** | **85** | **64** |
| 5 | Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | 10.Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | | | | | | | | | | |
| | | 11. Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba | | | | | | | | | | |
| **Jumla ndogo** | | | | **26,000,200,000** | **7,712,437,000** | **11,879,226,000** | **19,591,663,000** | **6,580,252,537** | **9,979,680,176** | **16,559,932,713** | **85** | **64** |
| 6 | Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi | 12.Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi | Tume ya Uchaguzi | 3,361,500,000 | 2,374,507,824 | 439,662,000 | 2,814,169,824 | **2,373,426,278** | 195,232,500 | **2,568,658,778** | **91** | **76** |
| 7 | Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | 13. Uendeshaji wa shughuli za kiutawala wa Tume ya Uchaguzi | | | | | | | | | | |
| | | 14. Uendeshaji wa shughuli za kiutawala wa Tume ya Uchaguzi | | | | | | | | | | |
| **Jumla ndogo** | | | | **3,361,500,000** | **2,374,507,824** | **439,662,000** | **2,814,169,824** | **2,373,426,278** | **195,232,500** | **2,568,658,778** | **91** | **76** |
| | **JUMLA KUU** | | | **57,669,700,000** | **14,131,394,824** | **29,917,158,512** | **44,048,553,336** | **13,095,605,701** | **25,661,674,238** | **38,757,279,939** | **88** | **67** |

**Kiambatisho Nam. 12**

**UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI MACHI, 2023**

| S/N | JINA LA PROGRAMU NDOGO | JINA LA MRADI | FEDHA ILIYOTENGWA KWA MWAKA | | FEDHA ILIYOTENGWA KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOPATIKANA | ASILIMIA YA MIEZI TISA | ASILIMIA YA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Shughuli za SMZ | Programu ya TASAF III | Wahisani | 17,546,457,000 | 13,159,842,750 | 9,298,768,246 | 71 | 53 |
| | | | SMZ | 100,000,000 | 75,000,000 | 25,000,000 | 33 | 25 |
| | **JUMLA** | | | **17,646,457,000** | **13,234,842,750** | **9,323,768,246** | **70** | **53** |

**Kiambatisho Nam. 13**

**UKUSANYAJI MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 – MACHI, 2024**

| S/N | IDARA/TAASISI | FEDHA ILIYOTENGWA KWA MWAKA | FEDHA ILIYOPANGWA KUSANYWA KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOKUSANYWA MIEZI TISA | ASILIMIA MIEZI TISA | ASILIMIA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 52,710,000 | 43,310,000 | 22,405,600 | 52 | 43 |
| 2. | Ofisi Kuu Pemba | 22,542,000 | 18,042,000 | 6,660,000 | 37 | 30 |
| 3. | Tume ya Uchaguzi | 10,000,000 | 7,100,000 | 4,657,000 | 66 | 47 |
| | **JUMLA** | **85,252,000** | **68,452,000** | **33,722,600** | **49** | **40** |

**Kiambatisho Nam. 14**

## MAPENDEKEZO YA MGAWANYO WA UKOMO WA BAJETI OMPR 2024/2025

| CODE | PROGRAMU NDOGO | MSHAHARA | OC | DEV SMZ | DEV WAHISANI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | OFISI YA FARAGHA | 1,241,644,100 | 607,504,000 | - | - | **1,849,148,100** |
| | IDARA YA SHEREHE | 312,595,584 | 1,219,771,004 | - | - | **1,532,366,588** |
| | IDARA YA URATIBU SHUGHULI SMZ | 735,708,420 | 1,344,881,000 | 100,000,000 | 30,220,108,070 | **32,400,697,490** |
| | OFISI YA URATIBU DOM. | 604,109,684 | 887,638,000 | 550,000,000 | - | **2,041,747,684** |
| | U/UTUMISHI | 1,118,473,802 | 735,912,000 | - | - | **1,854,385,802** |
| | IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTUMISHI | 306,339,628 | 199,903,000 | 4,500,000,000 | 204,000,000 | **5,210,242,628** |
| | PEMBA | 690,528,782 | 262,791,000 | - | - | **953,319,782** |
| | **Jumla ndogo** | **5,009,400,000** | **5,258,400,004** | **5,150,000,000** | **30,424,108,070** | **45,841,908,074** |
| | **RUZUKU** | | | | | |
| 201 | MAAFA | 942,200,000 | 793,400,000 | | 130,000,000 | 1,865,600,000 |
| 203 | UHAMIAJI | 0 | 23,125,000,000 | - | - | 23,125,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | **942,200,000** | **23,918,400,000** | **-** | **130,000,000** | **24,990,600,000** |
| | **JUMLA C01** | **5,951,600,000** | **29,176,800,004** | **5,150,000,000** | **30,554,108,070** | **70,832,508,074** |
| | BARAZA LA WAWAKILISHI | 10,837,401,000 | 20,035,999,000 | - | - | 30,873,400,000 |
| | TUME YA UCHAGUZI | 4,800,400,000 | 580,000,000 | - | - | 5,380,400,000 |
| | **JUMLA KUU OMPR** | **21,589,401,000** | **49,792,799,004** | **5,150,000,000** | **30,554,108,070** | **107,086,308,074** |